**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Tano – Tarehe 12 Juni, 2010**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

Naibu Spika (*Mhe. Anne S. Makinda*) Alisoma Dua

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2010**
**(*The Finance Bill, 2010*)**

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni kwa mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2009 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema tunaendelea na kazi yetu na tunao wachangiaji kama 20 nadhani wanatosha kwa muda wa saa za asubuhi. Halafu tunafikiri kwenye upande wa Mawaziri wajiandae kujibu hoja za Wabunge zilizotokea katika Wizara ya Fedha wale wanaohusika nazo kusudi Jumatatu tutakapokuja Waziri ana *wind up* itakuwa rahisi kuendelea na kazi na Mawaziri watakuwa hawahusiki na zile hoja kwenye Wizara zao. Kwa hiyo, watakuwa na nafasi siku ya Jumatatu wajiandaye.

Kwanza nilikuwa nimwite Mheshimiwa Suleiman Kumchaya halafu Mheshimiwa Charles Keenja.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi. Awali ya yote ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai mpaka leo ninapozungumza katika Bunge hili tukimaliza miaka 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Lulindi kwa ushirikiano wao walionipa katika kipindi chote cha miaka 5. Nawashukuru Mpindimbi, Chiwata, Marika, Nanjota, Chiungutwa, Mkululu, Lulindi, Lipumbulu, Mnavira na Kata yetu mpya Chikolopola, wamenipa ushirikiano mkubwa sana na ndiyo maana wameniomba na kuniruhusu nichukue tena fomu za kugombea ubunge mwaka 2010 na sintowaangusha hata kidogo. (*Makofi)*

Ningependa kuipongeza Wizara ya Fedha na Uchumi na Serikali yote kwa ujumla kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi chote cha miaka mitano (5) pamoja na kipindi hiki ambapo tunasoma Bajeti ya mwisho ya miaka mitano. Ningependa kuwapongeza katika maeneo yafuatayo, kwanza Elimu ya Sekondari. Katika kipindi hiki cha miaka mitano Serikali yetu ya CCM na wananchi kwa ujumla ilifanya kazi nzuri ya kueneza Shule za Sekondari katika kila Kata. Nilitoa mfano wangu mimi mwenyewe katika jimbo langu la Lulindi. Tulipokuwa tunaanza miaka 5 hii katika jimbo langu kulikuwa na Shule za Sekondari katika Kata 5 tu. Lakini hivi leo ninavyozungumza kwa nguvu ya Serikali wananchi na Mbunge wao na viongozi wengine tumeweza kujenga Shule za Sekondari katika kila Kata. Hakuna hata Kata moja ambayo haina Shule ya Sekondari. Hii ni hatua kubwa katika kuthamini elimu katika nchi yetu. Tunachoomba tuongezewe walimu, vitabu, maabara ili shule zetu hizi ziweze kutoa wanafunzi waliokomaa kielimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuipongeza Wizara ya Miundombinu na Serikali kwa ujumla, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kutengeneza barabara katika nchi yetu ya Tanzania. Mimi natoka katika jimbo la vijijini Lulindi, mpaka ninavyozungumza sasa hivi katika Bunge hili asilimia 90 ya barabara zimetengenezwa katika jimbo la Lulindi. Napenda kuipongeza sana Serikali na wananchi kwa ujumla kwa kuwezesha utengenezaji wa barabara hizi. Leo hii magari yetu ya korosho hayakwamikwami yanapita bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuipongeza Serikali katika eneo la zahanati. Hivi ninavyozungumza wananchi wa jimbo la Lulindi kwa kushirikiana na Serikali zao wanaendelea kujenga zahanati katika kila kijiji na zingine zimeshakamilika. Tunachoomba kwa Serikali kutuongezea Waganga kuwa na dawa ili wananchi wasiweze kupata taabu tena ya kutembea kilomita nyingi kufuata matibabu kama ilivyokuwa huko nyuma. Napenda sana kuipongeza Serikali katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kilimo ningependa kuipongeza Serikali kwa kuongeza fedha dhana yetu ya kilimo kwanza hapa ningependa kukumbusha *export levy* bado inatuletea matatizo haijakwenda katika Halmashauri. Tunajaribu kila njia lakini bado suala hili ni gumu sana. Tunaomba sana Serikali suala hili lipatiwe

ufumbuzi maana linawatia uchungu sana wakulima wa korosho ambao walitarajia kwamba wangeweza kupata fedha hizi kwa ajili ya kuendeleza mikorosho yao. Lakini tungependa kupongeza kwa kuongeza ushuru katika korosho ambazo tunapeleka nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa maji naiomba Serikali itimize ahadi yake. Suala hili nimelizungumza mara nyingi sana na Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Mwandosya na ametoa ahadi kwamba watafanya kila linalowezekana ili chanzo cha maji cha Chiwambo katika jimbo la Lulindi kiimarishwe kiweze kutoa maji katika jimbo la Lulindi na kisaidie mradi mkubwa wa Mbwinji ambao jana hapa ameuzungumza vizuri sana Mheshimiwa Mrope kutoka jimbo la Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimezungumzia suala la miundombinu. Mara nyingi ninapozungumza katika Bunge hili sisahau hata kidogo matumizi ya Bandari zetu ili tuweze kujenga uchumi wa haraka katika nchi yetu bandari ya Mtwara tunaomba sana.

Kwanza niipongeze Serikali kwa kuondoa *stiff doaring* ambayo inatoa ruhusa kwa meli yoyote kutia nanga pale, kushusha na kupakia bila ya kuwa na ushuru mkubwa. Tunaomba basi Serikali iongeze nguvu kuhakikisha kwamba bandari yetu ya Mtwara inafanya kazi kwa manufaa ya nchi hii na hasa ikizingatiwa kwamba tayari daraja la Mtambaswala limeshafunguliwa na Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Tayari pana biashara nyingi, tayari wenzetu wa Mozambique Kaskazini wanataka kuitumia bandari ile. Naomba sana hili lisiwekwe pembeni, litasaidia sana katika uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningependa pia nizungumzie bandari na barabara zetu hizi. Kwanza napenda kuishukuru Serikali kwamba inaendelea kumaliza kutengeneza barabara ya Dar es Salaam/Lindi/Mtwara kilomita 60 ili iweze kukamilika, nakushukuruni sana. Lakini pamoja na hayo bado Serikali itilie mkazo utengenezaji wa reli yetu ili iweze kutoa mchango mkubwa wa uchumi katika nchi yetu hasa tukizingatia kwamba nchi yetu inakwenda katika maeneo ambayo hawana bandari hata kidogo wanategemea bandari zetu hizi za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga lakini hawawezi kutoka kule kama reli yetu itakuwa bado haijakamilika kiasi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia tena kuwashukuru wapiga kura wangu wa jimbo la Lulindi na ninaamini kabisa kwa moyo wa dhati kwa kuwa tumeshirikiana vizuri basi hawatasita hata kidogo kunirudisha tena katika Bunge hili ili niendelee kuwatumikia kama nilivyowatumikia katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. CHARLES N. KEENJA**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nitoe mawazo kuhusiana na Bajeti yetu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii inaandaliwa katika kipindi kigumu sana. Mwaka jana tulikuwa na ukame tukawa na njaa, Serikali ikajitahidi na naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana na ikajitahidi kupambana na hali ile ya njaa na hakuna mtu aliyedhurika. Mwaka huu vile vile tulikuwa na mkanganyiko wa fedha katika dunia ambao umeathiri maendeleo yetu. Wahisani nao wakaleta ya kwao ya kutunyima fedha. Kwa hiyo, tunaandaa Bajeti hii katika kipindi ambacho ni kigumu sana. Naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Manaibu wake na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu kubwa sana ni vyanzio vichache sana vinavyoipa Serikali mapato na hatua tunazochukua ama tusizochukua ambazo zinasababisha wananchi wetu waendelee kuishi katika mazingira ya umaskini na ukosefu wa mahitaji mengi sana. Kwa hiyo nafikiri katika Bajeti hii na katika Bajeti zijazo ni muhimu sana kutilia mkazo uzalishaji katika kilimo, uzalishaji katika viwanda, uvuvi na kadhalika ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na maeneo mengi zaidi ambayo yanaweza yakachangia mapato ya nchi na mapato ya Serikali. Bila ya kufanya hivyo tutakuwa na matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukizungumzia suala la zana ya kilimo kwanza. Kwamba masuala ya kilimo tutayapa uzito ili yachangie katika kupunguza umaskini. Lakini hili pia linasaidia kuchangia katika kuongeza mapato ya Serikali.

Lakini ukiangalia vitendo vyetu vingi tunavyofanya haviendi huko. Tulikuwa na viwanda vya kutengeneza zana za kilimo *UFI* na KIZAKU vyote vimefungwa havikutengeneza hata kwanja la kufyekea. Sasa tuna gesi katika maeneo mawili makubwa katika nchi yetu ambayo tungeweza kutumia kutengeneza mbolea lakini bado sioni mipango madhubuti inayotumia rasilimali hii kutuwezesha kuzalisha.

Kwa hiyo, kuna haja Serikali kuchukua hatua za makusudi kurekebisha baadhi ya haya matatizo na kuweka utaratibu utakaowezesha wananchi wetu kwanza wakulima wadogo, wafugaji wadogo, wavuvi wadogo, wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi, kwa ukubwa zaidi na kwa kibiashara.

Lakini wakati huo huo kuhakikisha kwamba kuna kundi litakaloibuka watakaozalisha kwa ajili ya biashara zaidi kuliko kwa ajili ya kujilisha. Kwa hiyo, wazalishaji wakubwa zaidi katika kilimo, ufugaji na uvuvi. Tusipofanya hivyo tutaendelea kuwa na matatizo ya kuwa na vyanzio vichache sana vya mapato. Lakini baya zaidi tutaendelea kuudumisha umaskini miongoni mwa watu wetu na mateso yanayoendana na umaskini huu. Kwa hiyo, ningeomba sana hili tulitazame.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukirudi katika kilimo kwanza, mpaka sasa tunazungumzia kilimo kwanza lakini hatujaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba ile misingi ya kilimo kwanza inatekelezwa. Moja ni kuhakikisha kwamba sekta ya watu binafsi inashiriki katika kilimo. Kwa hiyo, katika kilimo kile kikubwa cha eka 200 na kuendelea ambazo zinaweza kuzalisha kibiashara.

Mimi nafikiri kama Serikali inataka kweli jambo hili lifanyike vizuri kuna haja ya kuunda Kamati ya watu binafsi na Serikali itakayoshirikiana kuweka utaratibu utakaohakikisha kwamba tunashirikisha sekta binafsi katika uzalishaji katika kilimo. Kazi ya Serikali sasa iwe nini? Mimi sioni Serikali ikawa ndio chombo kikuu kitakachoshiriki katika kukuza uzalishaji katika nchi hii.

Lakini itabidi Serikali iweke mazingira yatakayoiwezesha sekta binafsi kuwekeza. Iweke mazingira yatakayowezesha sekta binafsi kupata mahitaji yao ili sasa waweze kuwekeza na kuzalisha kwa wingi zaidi. Tusipofanya hivyo tutapata matatizo ambayo hayatatutoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tunabidi kulitazama ni suala la kuziba mianya inayotupotezea mapato na iko mingi sana. Katika hotuba ya Waziri ametaja baadhi ikiwa ni pamoja na magari mengi sana yaliyopo Serikalini ambayo uendeshaji wake ni wa gharama kubwa sana yanapelekwa kwenye magereji chini ya miti ambapo tunapoteza fedha nyingine ambazo wala hazihusiani na matengenezo na kadhalika.

Serikali ya awamu ya pili iliamua kupunguza magari hayo yabaki manne (4) kwenye kila Wizara. Yalipokuja mabadiliko nafikiri tukasahau kwamba kulikuwepo na misingi ambayo imeshawekwa. Kwa hiyo, tukarudi kule kule tulipokuwa. Kuna haja ya kuangalia ni nini tufanye kuhakikisha kwamba wafanyakazi wetu wanapata usafiri, lakini wakati huo huo kuhakikisha kwamba huu mzigo mkubwa sana unapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna maeneo mengi ambayo yanatupotezea mapato, Mashirika ambayo yanatupotezea mapato, Mashirika yanayoingiza hasara na nafikiri mengine ambayo sio ya lazima.

Mimi sina hakika kama tunahitaji Shirika la Ndege kwa sababu jitihada zetu zote za kufufua Shirika la Ndege zimeshindikana na tunapata hasara kwa sababu inabidi liendeshwe kutokana na Bajeti ya Serikali. Lakini tunahitaji Reli ya Kati, tunahitaji Reli ya Kaskazini itakayokwenda mpaka Ziwa Victoria, tunahitaji hata reli kutoka Mtwara itakayoenda mpaka Ziwa Nyasa. Ili kuhakikisha kwamba tunachukua mali zitakazokuja katika nchi hii kupeleka katika maeneo mbali mbali katika nchi jirani na wakati huo huo kila tunachozalisha kinasafirishwa kwa ufanisi ili kitoke nje ya nchi.

Kwa hiyo, kuna maeneo ambayo ni lazima kwa makusudi kabisa tuchague kuwekeza maeneo ya uzalishaji, miundombinu ya kiuchumi ambayo inatupa uwezo zaidi wa kuendesha nchi hii kwa ufanisi. Nina hakika kama tungetengeza hizi reli zikaenda mpaka Kigali, Bujumbura yakaenda mpaka *East Zaire* peke yake ingetosha kutupa mapato makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lazima tufike mahali vile vile tufanye maamuzi yenye manufaa kwa Taifa letu. Tuna madini ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia, Mwalimu aliamua yabaki ardhini mpaka tutakapokuwa na uwezo wa kuyachimba.

Lakini tumeamua kuyachimba kwa sababu tunafikiri wakati umefika. Kwa nini sasa hatutozi kodi madini yale ili tuweze kuwekeza kodi hizo katika maendeleo ya wananchi wetu. Dhahabu wakati migodi hii ilipoanzishwa bei ya dhahabu ilikuwa ni Dola 450 kwa wakia na sasa hivi ni Dola 1200 na ushehe hivi kwa wakia.

Kwa hiyo, mapato wanayopata ni makubwa sana kwa nini hatuwatozi kodi kwa kiasi hicho wanachopata cha ziada. Au *Stigler* ambao nao wana migodi ambayo wanachimba dhahabu na madini mengine wameamua kuwatoza kodi. Serikali ikaambiwa mkiwatoza kodi hawa wataaondoka, wakasema nawaondoke, hawakuondoka.

Nadhani sisi tukiwatoza kodi nina hakika hawataondoka watatupa tu mchango utakaotuwezesha kuendeleza nchi hii. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo tukiyafanya na tukiyafanya kwa ufanisi nina hakika kwamba hali yetu ya kiuchumi itaboreka, itakua kwa haraka zaidi na wananchi wetu wataondokana na umaskini huu ambao unakwaza sana maisha yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba, Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha vile viwanda vya mbolea vinafufuliwa mapema iwezekanavyo na tuanze katika mwaka huu. Vile viwanda vingine tulivyovibinafsisha ambavyo havifanyi kazi, Serikali ivichukue na ivibinafsishe upya au tuweke utaratibu mpya wa kiviendesha.

Nilikuwa naangalia runinga juzi nikasikia kwamba, sasa Shirika la Reli la Tanzania litaendeshwa na Watanzania wenyewe. Sisi siyo wa kwanza, Uingereza walibinafsisha Shirika lao la Reli likafika mahali likafanya vibaya sana wakalitaifisha wakaliendesha kama Serikali; na sisi tufanye hivyo hivyo. Tuhakikishe tunanunua injini na mabehewa ya kutosha ikibidi kwa mkopo halafu twende kazini.

Nina hakika tukienda kazini na tukahudumia nchi za jirani na mikoa yetu, tukaweza kuzalisha pamba kutoka Shinyanga na Mwanza kwa ufanisi hii reli italipa. Tukiendelea bila kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba njia zetu zote za uzalishaji zinatumika kikamilifu, tutapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda nizungumzie vijana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S. MSAMBYA**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu na nasema hapa kwa niaba ya wananchi; kwanza wa Kigoma Kusini na pili wa Mkoa wa Kigoma.

Nitajielekeza katika maeneo matano ambayo ni Kilimo, Uvuvi, Miundombinu, Mawasiliano na Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa Bajeti iliyowasilishwa hapa, imetilia maanani kilio cha mkulima mdogo mdogo hasa pale walipozingatia sehemu ya ushuru kwa vifaa vya kilimo. Ningeomba Serikali itambue kwamba, Kigoma ni moja ya mikoa sita iliyoko katika mkakati huu wa Kilimo Kwanza, kwa maana ya Ghala la Chakula la Taifa, lakini mbolea inawachelewa kuwafikia wakulima.

Mbolea ya kupandia inafika wakati wa kufikisha mbolea ya kukuzia. Ni vizuri basi Sekta inayohusika na jukumu hili, iangalie kwa misimu inayokuja mbolea hii inafika kwa wakati ili dhana ya kwamba tunatakiwa tuwe sehemu ya Ghala la Taifa la Chakula iwe na uhalisia wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia Kitabu cha Bajeti ya Mheshimiwa Waziri, sikuona popote pale ambapo mvuvi amezungumziwa kwa kina. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipoteuliwa, alijitangaza yeye ni mtoto wa mkulima na mimi ni mtoto wa mvuvi. Sisi kule Kigoma tunavua uvuvi mdogo mdogo na tuna zana duni sana, hatukuona popote ambapo Serikali imejielekeza kumtambua huyu mvuvi mdogo mdogo ama kwa njia ya mkopo au kwa njia nyingine yoyote ile.

Mbaya zaidi, mvuvi anayevua Ziwa Tanganyika yupo hatarini kuvamiwa na maharamia na wanyang'anyi kutoka nchi jirani. Tulitegemea Serikali ingetuwekea utaratibu wa kumlinda huyu mvuvi na zana zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende upande wa miundombinu; barabara na reli. Nianze na Reli. Tunayo Reli ya Kati. Sisi tunaotoka sehemu ambayo Reli hii ndiyo njia kuu ya usafiri, tumeteseka kwelikweli. Tulipata faraja kama wiki moja iliyopita tuliposikia kwamba, Serikali itatafuta namna ya kuiendesha reli hii yenyewe. Isifanye utaratibu wa kuiendesha tu, Serikali iendeshe kwa ufanisi zaidi. Reli ya Kati ni kiungo cha uchumi kati ya Tanzania na Burundi, Congo, Rwanda na Zambia.

Kwa hiyo, ingekuwa vizuri basi kabla hatujachukua uamuzi wa ubinafsishaji wa Shirika hili kwa mtu mwingine tena baadaye. Tuwatilie maanani hawa watu ambao ndiyo watakaoweza kuijenga reli hii. Mizigo inayotoka kwenye nchi hizi nilizozitaja, inaweza kabisa kuimarisha uchumi. Wakati mwingine tunakurupuka tu tunadhani kwamba, barabara zilizopo zinatosha; hatuna barabara za kutosha kusafirisha mizigo ya hawa jirani zetu.

Kwa hiyo ni vizuri tutakapochukua hatua sasa ya kuendesha reli hii, tutilie maanani kwamba kuna mzigo mkubwa sana unaotoka nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, twende kwenye suala la barabara. Tunashukuru kwamba, Barabara za Magharibi zimeanza kujengwa na tarehe 15 Mheshimiwa Rais anakwenda kuzindua barabara ambayo inajengwa kutoka Kigoma kuja Tabora, ambayo imefika sehemu inayoitwa Kidahu. Hii haitotosha kama mtazamo hautakuwa wa

kuiharakisha barabara hii ili iungane na Tabora na Tabora iungane na Dodoma. Hii ndiyo itakayoweza kuleta ufanisi mkubwa katika nchi.

Sasa lipo suala la mawasiliano, nashukuru nimeshawahi kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa sekta husika na wameniahidi na nadhani pengine katika kipindi cha wiki mbili wataalam watakuwa wamekwenda, lakini isiwe kusukumwa. Mwambao wa Ziwa Tangayika, mahitaji ya simu za mkononi ni makubwa sana.

Kuna pesa zimelala pale watu wanatakiwa wazitumie, lakini mashirika haya ya kutoa simu za mkononi yanasuasua. Kwa hiyo, ninaihimiza Serikali ione kuwa kule nako ni sehemu ya Tanzania, wale walioko kule wanatakiwa kuwasiliana na watu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wananchi wa Mkoa wa Kigoma wameshtushwa sana na suala la Nishati ya Umeme. Kuna suala la umeme ambao unatakiwa kuzalishwa pale Igamba, Mto Malagarasi, Uvinza. Wameshtushwa kwa kuambiwa kwamba, vyura vimekuwa na thamani zaidi kuliko binadamu kwamba, ule mradi uliokuwa uhudumiwe na MCC unasitishwa eti kwa kuthamini vyura. Kwamba, vyura wale ni *rare species* ambazo haziwezi kupatikana mahali pengine.

Vyura waliopatikana kutoka Kihansi walipelekwa Marekani na wakarudi au wanatarajiwa kurudi. Sioni kama vyura wanaweza wakazuia umeme usizalishwe au wakawanyima watu kupata nishati ambayo italeta maendeleo kwa wananchi wa sehemu husika. Nilikuwa naiomba Serikali ifikirie upya suala la kusitisha mradi huu wa umeme pale Igamba Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza haya, naamini Serikali imesikia na hasa kwa hili la umeme, itatafuta namna ya kutupatia Kigoma umeme wa uhakika mbali na huu unaokatika kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mwenyenzi Mungu, kwa yote ninayoyajua na nisiyoyajua. Nakushukuru wewe binafsi, kwa kunipa nafasi ya kusimama hapa.

Tatu na kwa namna ya pekee kabisa, nawashukuru sana wapigakura wangu wa Jimbo la Chambani kwa jinsi walivyoridhika na utumishi wangu kwa kunipa kura nyingi sana na hii inaonesha kwamba, kwa uamuzi huo na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitarudi Bungeni mwaka 2010 – 2015; *Inshallah*.

Semeni *Inshallah. (Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ruhusa ni ya Naibu Spika, siyo unasema wewe. (*Kicheko*)

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, katika kuchangia Bajeti hii inabidi tujiulize; Bajeti hii ya 2010/2011 ina utofauti gani na Bajeti iliyopita katika kuboresha maisha ya Watanzania ambao kila uchao yanakuwa magumu zaidi?

Mimi nakubaliana sana na Maoni ya Bajeti Mbadala ya Upinzani kwamba, Bajeti hii ya Mwaka 2010/2011 siyo tu itakuwa kitanzi cha wapigakura wakati uchaguzi ujao kwa Chama cha Mapinduzi, lakini vilevile haina jipya na kama alivyosema Mbunge mmoja wa CCM kwamba, hii ni Bajeti ya Ulaji tu. Haiboreshi kabisa maisha ya wananchi wa hali ya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza Bajeti ya Tanzania, lazima uzungumzie asilimia 80 ya Watanzania ambao wanaishi vijijini. Lazima uzunguzmie kazi zao ambazo ni kilimo ufugaji, uvuvi na kadhalika. Nitalizungumzia suala moja tu la kilimo. Takwimu tulizonazo zinaonesha kwamba, kilimo cha Tanzania kinasuasua. Kwa mfano, mwaka 2006 kilikua kwa asilimia 3.8, mwaka 2007 kilikua kwa asilimia 4, mwaka 2008 kilikua asilimia 4.6 na mwaka 2009 kilikua kwa asilimia 3.2. Kwa ukuaji huu wa asilimia ndogo kiasi hiki, bila shaka haiwezekani kuondoa umaskini wa Mtanzania. Kwa sababu ili umaskini uondoke ni lazima kilimo kikue angalau kwa asilimia angalau kumi kama tulivyokubaliana katika Nchi za SADC; vinginevyo, mizizi ya umaskini itakuwa inaendelea kukua kila siku. Asilimia hizi haziondoi umaskini hata kidogo. Tusisahau kwamba, kuna ahadi ya Chama cha Mapinduzi hapa kwamba, kilimo kinakua kwa asilimia 20; ahadi ile iko wapi? Nafikiri ni aibu tupu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ambazo zinaelezwa na Serikali ya Awamu ya Nne ni kwamba, uwekezaji mdogo. Kweli uwekezaji ni mdogo kwa sababu kwanza, kuna urasimu mkubwa katika uwekezaji, lakini vilevile nani atawekeza katika nchi ambayo Miundombinu ya Kilimo ni mibovu sana.

Wawekezaji wa Tanzania ni wale ambao wako kwenye madini, kwa sababu kwenye madini ni kama shamba la viazi, unakwenda na jembe lako unafukua unaondoka zako; lakini kwenye kilimo huwezi kuwekeza kwa haraka kwa sababu miundombinu yake ni mikubwa. Tunataka wawekezaji wakubwa kwa ajili ya kilimo cha biashara.

Tuwasaidie wakulima wadogo wadogo kwa sababu hawawezi kununua madawa, mbolea wala mbegu bora na upatikanaji wa pembejeo hizi ni mgumu sana kwa baadhi ya Wilaya na watu, siyo watu wote. Kwa hiyo, nafikiri Serikali lazima iwekeze katika ruzuku hizi ili wote wafaidike.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais Kikwete alisema, Morogoro itakuwa Ghala la Taifa ili kulisha Tanzania nzima. Ni aibu toka 2006 mpaka leo hakuna kilichofanyika; hakuna Ghala la Taifa popote! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo Kwanza kilipokuja hapa katika Bajeti iliyopita tulisema hii ni siasa tukadharauliwa; lakini hebu nioneshe ni iko wapi Bajeti ya Kilimo Kwanza? Hili ongezeko la Bajeti, kwa mfano, asilimia 35 ya Sekta nzima ya Kilimo; hii

kweli ni Kilimo Kwanza? Huku ni kutaniana. Bado suala la Kilimo Kwanza halikutiliwa maanani na kwa hiyo Kilimo cha Tanzania hakiwezi kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona Serikali hii ya Awamu ya Nne ina ukiritimba mkubwa kuhusu soko la mazao ya wakulima. Wakulima wanajitafutia kila kitu wenyewe; pembejeo wenyewe, madawa wenyewe na mbegu wenyewe, lakini wakati wa kuzalisha wanaambiwa uzeni pale msiuze hapa. Nina mifano miwili mizuri sana; hivi sasa kule Lindi wakulima wa ufuta wanaambiwa lazima wawauzie Vyama vya Msingi vya Ushirika ambavyo vinanunua ufuta kwa shilingi 750 kwa kilo tena kwa mkopo, lakini wakati wa kulima hakuna aliyewashughulikia.

Kuna wanunuaji binafsi wanataka kununua kwa shilingi 1,200 kwa kilo lakini Mkuu wa Mkoa anasema lazima wauziwe Vyama vya Ushirika. Huu ni ukiritimba na ukandamizaji mkubwa wa wakulima wetu. Hatutakubali kuona wakulima wetu wanadhalilishwa kiasi hicho. Lazima Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ufuatilie hili na kuona wakulima wanauza ufuta wao kwa bei muafaka.

Nina mfano mwingine wa kilimo cha mpunga. Tumekwenda kule, wakulima wanalima mpunga mwingi sana, lakini walipovuna wakaambiwa msiuze nchi za nje.

Walikuja wanunuzi kutoka Malawi, lakini hawakuweza kununua. Baadae Serikali ikasema sasa uzeni nje. Walipotaka kuuza wale wanunuzi kutoka Malawi wakasema tumeshapata soko sehemu nyingine.

Nadhani hii tabia ya kusema wakulima msiuze kwa ajili ya *food security; food security* ya nani? Mkulima analima kwa manufaa yake kwanza halafu ndiyo anaangalia Taifa. Lazima wakulima waruhusiwe kuuza mazao yao popote na kwa faida. Vinginevyo, Serikali iwafidie kama haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya *D by D* siyo mbaya lakini imekosa usimamizi na hii haiwezi kufanywa na Serikali ya CCM. Waziri amekubali katika kitabu chake, ukarasa wa 23, amesema kwamba, fedha nyingi zinazotumiwa kwenye Halmashauri hususan fedha za maendeleo, zimekuwa zikirundikana kwenye akaunti bila kutumiwa kwa wakati.

Serikali inajua kwamba, haina uwezo kabisa; Halmashauri hazina uwezo wa kitaalam wala hazina uadilifu, ndiyo maana unaona katika Halmashauri kuna upotevu mkubwa sana wa fedha za Serikali. Hapo Bagamoyo juzi tu Waziri Mkuu aliwasimamisha Watendaji Wakuu wa Halmashauri ya Bagamoyo, kwa sababu ya ubadhirifu wa fedha za Serikali.

Kwa hiyo, nafikiri iko haja kwa sababu asilimia 75 ya fedha za miradi zinakwenda kwenye Halmashauri, ni fedha nyingi sana; kwa nini Serikali haiweki uzito kwa kuweka wataalam wenye uwezo na waadilifu ili Halmashauzi ziweze kufanya kazi muafaka?

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Kupeleka Madaraka katika Halmashauru *(D by D)* ni nzuri lakini haiwezi kamwe kusimamiwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi angalau nichangie kwenye Bajeti hii ya Serikali. Baada ya kukushukuru kwa kunipa nafasi, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wewe Naibu Spika na Wenyeviti wetu, kwa jinsi mnavyoliendesha Bunge hili kwa viwango. Ninaweza kusema Bunge la Historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika baada ya kushukuru, napenda niwashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Morogoro Mjini, kwa jinsi wanavyonipa moyo katika kipindi chote nilichokuwa katika madaraka haya na kutekeleza majukumu yangu. Ninapenda niwahakikishie kwamba, Mungu akipenda kama nitarudi katika kipindi kijacho, nitawafanyia mambo makubwa sana, kwa sababu sasa nimeshapata uzoefu wa kutosha katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimpongeze sana kaka yangu, Waziri wa Fedha, kwa jinsi alivyowasilisha Bajeti hii; kwanza, kwa kina lakini kwa kutoa vipaumbele katika nchi yetu. Kwa kumpongeza yeye pia napenda niwapongeze Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Makamishna, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda nijikite kwenye Kilimo. Kilimo ni uti wa mgongo katika nchi yetu na ninaishukuru Serikali kwamba, kwa mwaka huu wameongeza fedha kwenye Wizara ya Kilimo ukilinganisha na shilingi bilioni 666.9 za mwaka 2009 na mwaka huu wataweka shilingi bilioni 903.8, ambayo ni sawa sawa na ongezeko la asimilia 35.8. Tukitaka kuendelea katika kilimo ni vizuri tukajikita katika kilimo cha umwagiliaji ili tuweze kuwa na mafanikio.

Kutegemea mvua hizi za Mwenyezi Mungu, ambazo hazina uhakika, kwa kweli hatuwezi kwenda popote. Ushauri wangu katika kilimo cha umwagiliaji, tujikite katika maeneo machache ambayo yana mvua au yana maji ya kutosha ili miradi hii ambayo tunaianzisha ya umwagiliaji na kama inavyofahamika, miradi ya umwagiliaji ni miradi yenye gharama kubwa; ni vizuri tukaanzisha sehemu chache ambazo miradi hii inaweza ikaisha na ikaleta manufaa kwa wananchi kuliko kusambaza miradi katika Mikoa mbalimbali na matokeo yake ni kwamba, pesa ni kidogo miradi hiyo haiwezi kwisha. Kwa hiyo, hatuwezi kupata mafanikio yoyote; matokeo yake tunapiga *mark time.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni Mkoa wa Morogoro: Mkoa huu una maji, una mito mingi, mito zaidi ya 143 ambayo haikauki kwa mwaka. Kwa hiyo, ndiyo sehemu ambayo ingekuwa ya kuwekeza katika miradi ya umwagiliaji na kwa bahati nzuri, Mkoa huu ni Ghala la Taifa la Chakula, kwa hiyo ni vizuri tuka-*focus* kwenye Mkoa wa Morogoro pamoja na Mikoa mingine ambayo ina maji kama Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wetu wana matatizo makubwa sana. Sasa ningeishauri Serikali kwamba, ijikite katika pembejeo za kilimo. Kwanza, naishukuru Serikali katika mwaka uliopita wamejaribu sana kugawa mbolea kwa kutumia vocha ili kuwapunguzia gharama wakulima. Hata hivyo, ningeomba Serikali iongeze juhudi kwa mwaka huu kuongeza vocha ziwe nyingi zaidi ili ziwafikie wakulima walio wengi. Pembejeo hizo, ni mbolea pamoja na dawa na dawa hizo, ziko dawa za kuua wadudu kwenye mazao, lakini pia kuna dawa za kuua majani. Sasa, ningeiomba Serikali, katika mbolea, dawa za kuua wadudu na dawa za kuua majani, iondoe ushuru kabisa ili kusudi bei iwe nafuu wananchi wawe na uwezo wa kununua hizi dawa ili kuweza kuhudumia mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; ni kwamba pia Serikali ingewasaidia wale wananchi wenye uwezo waweze kuwakopesha matrekta ili na wenyewe waweze kuwakodisha wakulima ambao hawana uwezo ili waweze kulima. Nasema hivyo kwa sababu gani? Matrekta yakiwa ya watu binafsi, kwanza yatatunzwa vizuri na yatachukua muda mrefu na kuhakikisha kwamba nchi yetu inasonga mbele kuliko matrekta haya yakiwa ya Serikali kwa sababu kunakuwa hakuna mtu wa kuyatunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kubwa katika matrekta ni kwamba, kuna urasimu mkubwa sana wa kupata matrekta. Kwa mfano, pale Morogoro kuna Mzee wangu mmoja ameomba trekta sasa miaka miwili. Ametimiza masharti yote ya kuomba trekta, lakini mpaka leo trekta hajapata. Na mimi nashangaa, *TIB* mwaka jana miezi ya mwishoni tuliwapa bilioni 19 kwa sababu ya pembejeo za kilimo, sasa nashangaa kwamba urasimu unakuwa mkubwa, siwezi kuelewa ni kwa sababu gani. Naiomba Serikali iliangalie sana jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; naomba sasa nizungumzie suala la watumishi. Watumishi ni watu wanaopata matatizo, wenye shida kubwa sana katika maisha yao, hasa watumishi wa Wizara ya Elimu na watumishi wa Afya. Naishukuru Serikali kwamba mwaka huu imewaongezea mshahara, pamoja na kuwapunguzia kodi. Sasa, ningeshauri Serikali kwamba, mwaka hadi mwaka iongeze kuwapunguzia kodi kwa sababu gani, kuwaongezea mishahara peke yake haitoshi kwa sababu, inapoongezwa mishahara, maana yake na bidhaa zote zinapanda, kwa hiyo hawaoni hata ile faida ya mishahara yao kupanda. Lakini, kama wakipunguziwa kodi, ni bora zaidi kwa sababu watakuwa na kitu chochote ndani ya mikono yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeomba wafanyakazi hawa wasaidiwe kujengewa nyumba za watumishi, iwe kama motisha. Kwa sababu wafanyakazi wa Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu ndio wao wengi wanapangwa sana vijijini ambako hakuna huduma za nyumba. Kwa hiyo na wao wangejengewa nyumba hizi ili kusudi waweze kupata motisha, waweze kufanya kazi zao kwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naomba sasa nizungumzie jambo la uchafuaji wa mafuta ya magari. Jambo hili linasikitisha! Utakuta sasa hivi magari mengi yanaharibika kwa sababu ya mafuta ambayo yanachanganywa na mafuta

ya taa. Ni hatari! Mimi binafsi gari langu hivi ninavyozungumza limeharibika pampu kwa ajili ya mafuta ya kuchanganywa. Lakini, baya zaidi ni pale niliposikia juzi kwamba na magari ya Ikulu yanayombeba Mheshimiwa Rais na yenyewe yameshindwa kuwaka kwa sababu yamechanganyiwa mafuta. Kwa bahati nzuri magari haya yana *sensor*, ukiweka mafuta ya kuchanganya yanajijua yenyewe kwamba kuna mafuta yamechanganywa, hayawezi kuwaka. Lakini, kama ni magari ambayo hayana *sensor*, maana yake yatawaka, yatatembea na matokeo yake ni magari haya kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni jambo la kutisha, ni vizuri Serikali ikaliwekea kipaumbele. Kwa mfano, wenzetu Burundi, dereva akichanganya mafuta anawekwa ndani na wiki mbili zilizopita wako Watanzania zaidi ya watano, wamefungwa miaka mitano mitano Burundi na magari yakaachwa huko, tajiri ndiye akaenda kuchukua magari yake arudishe huku. Lakini, nashangaa sisi magari yanachanganywa, sijui *EWURA* wako wapi na *EWURA* ndio tumewapa majukumu haya. Kwa mfano, katika barabara hii ya Dar es salaam maeneo ya Kibaha, kila kilomita moja utakuta kuna kituo au kuna jengo ambalo kazi yake ni ya kufanya chakachua.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuweza angalau kutoa mawazo yangu katika kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa kuleta bajeti hii ambayo kwa kiwango kikubwa sana imeweza kumlenga moja kwa moja mwananchi hasa wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ukiiangalia kwa undani zaidi, utaona kwamba mwananchi yule ambaye ni wa kipato cha chini ameweza kuguswa kwa sababu zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na asilimia ile nyingine iliyobaki ni ya wafanyakazi. Kwa mujibu wa bajeti hii wakulima kwa kweli wameweza kuguswa katika nyanja nyingi sana; tukianzia na pembejeo za kilimo na masuala yote yanayohusu kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuzungumzia sana kuhusu suala hili hasa katika upande wa usimamizi wa hizi pembejeo. Serikali katika bajeti hii imeamua sana kumlenga mkulima katika kumsaidia kumwinua kutoka pale alipo, kwa sababu tunajua mkulima akisaidiwa, hata na jamii nyingine za wafanyakazi pia na zenyewe zitainuka na umaskini pia utapungua kwa sababu lengo zima ni kumsaidia Mtanzania kumtoa kutoka pale alipo ili aweze kupiga hatua kwenda hatua inayofuata katika kuboresha maisha yake ya kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatizo kubwa ambalo naliona ni kwamba, mipango ni mizuri sana, lakini naomba sana kuisisitizia Serikali, mipango hii mizuri iendane na watu bora ambao wataweza kusimamia yale yote ambayo Serikali inapanga. Nasema hivi kwa sababu, hivi karibu kama tunavyofahamu Serikali imeibua Mkakati wa Kuinua Kilimo kwa kuwa na kauli ya Kilimo Kwanza. Katika miezi miwili, mitatu tumekuta kuna matatizo mengi sana, Watendaji wetu, Wakurugenzi, Viongozi katika

Halmashauri, Viongozi katika Serikali za Mitaa, Vitongoji, Madiwani, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, wengi wamekuwa wakikabiliwa na matatizo kutokana na aidha kutokuwa waaminifu au kutokufanya kazi ya usimamizi bora katika suala la pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwamba, Serikali kwa sababu inajua kwamba lengo lake ni kumwinua mkulima kutoka katika hali ya umaskini ili kuboresha maisha yake ili hatimaye yeye kama akiwa na watoto waende shule, akiwa na ndugu kama wanasoma, akiwa na watu wote kama ni madaktari, kama ni mtu aliyesomea udaktari, kama ni wanafunzi, kama ni fani zingine zote ziweze kuboreka. Lakini mambo haya yote hayawezi kufanikiwa ikiwa kama tutakuwa na viongozi ambao hawaendani na dhana hii nzima ya Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeamua kutoa pesa nyingi sana kutoka Serikali kwenda kule chini kwenye Halmashauri za Wilaya. Lakini, je, ni kwa kiwango gani tunao viongozi kule kwenye ngazi ya Halmashauri ambao kweli ni waaminifu na ambao kweli wataweza kutimiza malengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana suala hili Serikali ifanye maamuzi magumu, tuangalie, mtu anaweza akawa na sifa nzuri, anaweza akawa na vyeti vizuri sana, lakini suala la uaminifu na kuchapa kazi siyo makaratasi peke yake! Kuchapa kazi ni kuleta matokeo yanayotegemewa. Sasa wewe usiwe kwamba mimi ni msomi sana, mimi nimechaguliwa nimekuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa au hata Waziri au nafasi yoyote, ukaona kwamba hapa mimi nilikuwa nastahili na hapa ndiyo nimefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujitahidi sana, viongozi hawa kama tunataka kuendana na malengo na matokeo yale ambayo tuliyatarajia, hawa viongozi katika nafasi zote nchini wawe ni watu ambao wanaendana na malengo ambayo Watanzania wengi wanayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda leo ni mdogo sana, nasikitika sana! Suala lingine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza ni kuhusu viongozi kufanya maamuzi. Lipo tatizo la Tanzania kutofanya maamuzi. Katika sehemu yoyote, katika nchi yoyote, wewe ukiwa kama ni Mkurugenzi, au ni Meneja, au kama kiongozi yeyote katika nafasi yoyote, usipofanya maamuzi, mtu yeyote ukiwa katika sehemu ya mamlaka, usipofanya maamuzi, wewe utaonekana mwema milele kwa sababu watu watakuwa hawajui wapi unaweza ukakosea na wapi unaweza ukapatia. Sasa hivi Tanzania imeibuka tabia ya kusema kwamba Mkurugenzi fulani ameteuliwa, lakini huyu unajua siyo mzungumzaji sana, yeye ni mtalaam sana wa kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hatuhitaji viongozi watalaam wa kuandika, tunahitaji viongozi ambao wanaweza wakafanya maamuzi, tunahitaji viongozi ambao wanaweza wakakaa na kufanya mambo ambayo sisi Watanzania yatatuondoa kutoka hapa tulipo na kupiga hatua kutokana na hali ya umaskini tuliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala lingine, ni kwamba viongozi hawa hawa matatizo waliyonayo, hawafanyi maamuzi, lakini vikao vya kujadili matatizo ni vingi sana, maamuzi ni machache. Lakini, licha ya hivyo, kuna vikao vingine vya kujadili maamuzi. Hii nchi haiwezi kwenda katika hali hiyo! Vikao vya kujadili matatizo vifanyike, vikao vya kuamua vifanyike, baada ya hapo iwe ni utekelezaji, siyo vikao vya kujadili maamuzi. Michakato imekuwa ni mingi sana ya kujadili vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho kabisa, naomba kwa heshima ya pekee kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa heshima ya pekee kumpongeza Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa John Chiligati kwa uamuzi mmoja mkubwa sana alioufanya. Uamuzi wa kumtoa mtu kutoka kwenye *private sector*, kumwingiza kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *National Housing* tena kijana. Naipongeza sana Serikali kwa sababu wafanyakazi wetu wengi, Wabunge wengi wamekuwa wakisimama wanalalamikia sana tatizo kwamba watu hawafanyi kazi, watu wamekaa tu, Serikalini huku ni kweli watu wamezidi kukaa na wamezidi kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano huu, ni kwamba Serikali sasa iendelee kuchukua watu kutoka kwenye *private sector*, kuwaingiza katika Serikali, tuweze kupata mawazo mapya na kwa kweli hata na wao wanaamini, kwa sababu kijana huyo ameingia pale, baada ya kuingia, kikao chake cha kwanza, kila mtu, mategemeo aliyokuwa nayo yalikuwa ni tofauti, aliwashangaza. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi huu na hii itawashitua hata wale wafanyakazi ambao wako Serikalini, tusifanye yale mambo ya *business as usual*. Wewe umekaa pale, “mimi nilikuwa Kaimu Mkurugenzi”, basi nafasi ya Ukurugenzi ikitokea nitapandishwa mimi. Hiyo itasaidia na imesaidia, watu sasa hivi waanze ku-*pull up their socks*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, naomba kuzungumzia suala moja, huu ni mwaka wa Uchaguzi, 2010 tunaingia kwenye uchaguzi, Waheshimiwa Wabunge wengi sana hapa watarudi kwa sababu wamefanya kazi nzuri sana. Lakini, vile vile ambacho napenda kuzungumzia…. *(Makofi)*

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, juu ya yule mtu wa *National Housing* una *interest* yoyote ile, mbona huku-*declare*, unajuaje mambo ya ndani? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi na mimi kutoa mchango wangu kwenye hotuba hii ya bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa kunipa ushirikiano mkubwa kwa kipindi kifupi hiki nilichokuwa nao na nawashukuru kwamba wananialika nirudi tena kwenye mchakato

mwezi wa nane ili tuhakikishe sasa tunaingia kwa kishindo na kufanya kazi yetu kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitoe pongezi kwa Waziri wa Fedha na timu yake nzima kwa kutuandalia hotuba hii kwa sababu hii inatuwezesha angalau kujadili kuona tumefika wapi na tunataka kwenda wapi. Kwa namna ya pekee, napenda nimpe pongezi Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa kazi nzuri anayofanya. Yako mengi ambayo tunayaona, lakini nitoe mfano wa machache tu. Nilifurahi sana jana niliposikia ndugu yangu, rafiki yangu Mheshimiwa Zitto Kabwe akifanya jitihada kuona namna gani naye anaweza kuhusishwa na yale mafanikio yaliyotokea Chuo Kikuu cha Dodoma. Nikasema hii ni ishara kwamba pale mambo yanakwenda vizuri. Nampongeza sana Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hotuba: Mchumi mmoja anaitwa Hernando De Soto ambaye alishirikiana nasi kutengeneza huu Mpango wa MKURABITA, alisema wakati huo kwamba asilimia 98 ya shughuli za kiuchumi nchi hii zinafanyika nje ya mfumo wa sheria, na asilimia 89 ya *properties* zote nchi hii ziko huko nje ya mfumo wa sheria, na akasema kwa ujumla wake anaona kwamba asilimia 90 ya shughuli zote za kiuchumi nchi hii zinafanyika nje ya mfumo wa sheria, kwa hiyo hakuna namna ambapo Tanzania inaweza ikaepuka kuendelea kuwa kwenye huu mzunguko wa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini, jana wakati wa hotuba nilifurahi sana pia kusikia Mheshimiwa Waziri wa Fedha anagusia hiyo changamoto anaposema kwamba "moja ya changamoto zilizopo ni kwamba sehemu kubwa ya shughuli zinazohusiana na uchumi wetu zinafanyika nje ya mfumo wa sekta rasmi na kwamba mapato ya ndani hayawiani na mahitaji ya kugharamia shughuli zetu kwa sababu hiyo ni kwamba, shughuli nyingi za uchumi zinafanyika nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya ya kusikia sentensi hiyo ya kwenye hotuba ya Waziri, nilikimbilia kwenye maktaba yetu pale, nikajaribu kuangalia hotuba nyingine zote za Mawaziri wa Fedha kuanzia mwaka 1999 mpaka ile ya jana, nikagundua kwamba changamoto hii imekuwa inarudiwa mwaka hadi mwaka, kuanzia hotuba ya 1999, 2000 mpaka ya jana zinarudiwa. Lakini ukisoma mikakati inayofuata baada ya changamoto hiyo kutajwa, utagundua kwamba mikakati hiyo inajikita kwenye kuangalia namna gani ya kutatua matatizo ya ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo vile vile, lakini haigusi kabisa vyanzo vipya kama ambavyo wamesema wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, ningependa pamoja na kutambua mchango ambao tunaweza tukaupata kwa kiwango kikubwa kutokana na vyanzo vipya ambavyo tayari vipo kwenye mfumo rasmi kama wenzetu walivyotamka; mambo ya samaki, madini na kama hayo. Ningependa nijikite zaidi kwenye vyanzo ambavyo bado hatujaweza kuviondoa kwenye mfumo usio rasmi kuviweka kwenye mfumo rasmi. Kwa sababu, kama ukubwa wa tatizo ni asilimia 90 kama anavyosema mwenzetu Hernando De Soto, pale tuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitarajia, kwa sababu tumekuwa na hii MKURABITA kwa miaka kadhaa sasa, nilitarajia hotuba zetu za bajeti kila mwaka ziwe zinatuambia, kutokana na shughuli zetu za mpango wa MKURABITA, ni watu wangapi wanaondoka kwenye mfumo usio rasmi wanaingia kwenye mfumo rasmi kwa faida yao wenyewe, lakini na kwa faida ya Taifa kwa maana ya kuongeza wigo wa ukusanyaji wa kodi. Hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kuangalia kwenye viambatanisho vya hotuba zetu zote kunzia mwaka 1999, 2000 mpaka jana, hakuna mahali ambapo tunaona namna gani wajasiriamali au watu wanaoshughulika kwenye shughuli za uchumi wanahama kutoka kwenye mfumo usio rasmi kuingia kwenye mfumo rasmi ili wafaidike na ili wigo wa walipa kodi uongezeke ili tuweze kujibu mahitaji ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona hilo ni tatizo na ningeomba tuliwekee mkazo wa kutosha. Tuanze kuweka *quantification* kila mwaka kwamba sasa mwaka huu watu kadhaa wamehama kutoka kwenye mfumo usio rasmi na wameingia kwenye mfumo rasmi na hapo ndiyo tutakuwa tunaweza kupima matokeo ya MKURABITA kwa namna iliyo sahihi zaidi. Vinginevyo, MKURABITA tutaambiwa tunafanikiwa, tunafanya vizuri lakini matokeo hatuyaoni. Kwa hiyo, naomba tuweke *quantification* kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwa kupitia hizo hotuba kumi za miaka kumi iliyopita nimegundua kwamba hivi viambatanisho vinakuwa havina *standard* kwa hiyo hata wale wafuatiliaji ambao wangependa kuona kama tumepiga hatua inakuwa ni vigumu. Ni lazima tuwe na baadhi ya viambatanisho ambavyo ni vya msingi tuvione kila mwaka ili tuweze kuona kwamba tunapiga hatua halafu vile viambatanisho ambavyo vinaendana na hali halisi ya mwaka huo vitakuwa vya nyongeza kwa hiyo, naomba nalo tulifanyie kazi tuone namna gani tunaweza tukaipima Serikali na kuwaambia kwamba hapa tunafanya vizuri na hapa hatufanyi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ningependa kuongelea vipaumbele vya bajeti ya mwaka huu imeguswa kuwa kipaumbele kimojawapo ni Uchaguzi Mkuu. Ni jambo jema kwamba ni lazima tuwe na hiyo shughuli kubwa ambayo ndiyo inatengeneza Serikali na tuendelee kufanya shughuli zetu lakini ni namna gani tutaondokana na hili suala la bajeti ya mwaka mmoja wa mwisho kuwa ndiyo inabeba mzigo wa Uchaguzi Mkuu, Wachumi wapo, mimi siyo Mchumi lakini najua wapo wanaweza kufanya kazi hiyo tuone ni namna gani tunaweza huo mzigo tukausambaza kwa sababu hii ni shughuli ambayo inafahamika kuwa itakuwepo kila baada ya miaka mitano.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke utaratibu ambapo huo mzigo wa shughuli za Uchaguzi Mkuu tunausambaza ili bajeti ya mwaka mmoja isiathirike. Kwa mfano, ukichukulia kama sekta ya Afya yapo mambo ambayo ukipunguza kwa kiwango kikubwa ni wazi itakuwa ile *trend* umei-*disturb* na ukii- *disturb* mwaka unaofuata utalazimika kurudi hatua nyuma na kuanza upya kwa hiyo, tutafute namna ambavyo huu mzigo tunausambaza unatazamwa kwa upana wake kwamba kuanzia sasa tunajiandaa kwa

Uchaguzi Mkuu wa 2015 na tunafanya hivi na vile na mwisho wa siku bajeti ya mwisho haibebi mzigo peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika miongoni mwa maamuzi yaliyofanyika napenda sana kupongeza uamuzi wa sasa kuanza kutenga pesa kwa ajili ya Utafiti huu ni uamuzi makini. Huu ni uamuzi makini kwa sababu Dunia inaongozwa sasa hivi na ushahidi bila kuwa na utafiti hatuwezi kuwa na ushahidi wa kutuwezesha kufanya maamuzi lakini pia nitoe angalizo, tunao ugonjwa na tatizo la kufanya tafiti ambazo hazifiki kwenye kutuletea masuluhisho kwenye matatizo ya maisha yetu. Kwa hiyo, tutenge pesa kwa ajili ya tafiti lakini tuweke mkakati ni namna gani matokeo ya tafiti hizi yatatumika na kuweza kujibu mahitaji ya maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifikia hapo naomba kuunga mkoa hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nishiriki katika mjadala huu wa bajeti yetu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi na wasaidizi wake wote, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na wote waliohusika katika maandalizi ya bajeti hii. Ni fasaha kabisa pamoja na mapungufu ya fedha ambayo yanatukabili kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimevutiwa na sera ya matumizi kwamba Serikali itaendelea kuongeza ufanisi katika kusimamia fedha za umma na hasa ikilenga katika maeneo ambayo yanalenga kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato. Hiyo ni sera nzuri sana ikisimamiwa kwa malengo ya kuondoa matumizi mabaya ya fedha chache tulizonazo. Utekelezaji wa bajeti hii unaweza ukaleta tija katika vipaumbele saba ambavyo nina viunga mkono mlivyovianisha Miundombinu, Kilimo, Elimu, Afya, Maji, Nishati na Utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Muleba kusini napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu nimepata fursa ya kuchangia kwenye hotuba hizi za bajeti tano bila kukosa na naomba Mwenyezi Mungu niweze kuchangia tano zingine zijazo. Kwa hiyo, nawashukuru wananchi kwa kunipa ushirikiano wa kutosha na Serikali katika mambo ambayo tumeweza kufanya. Serikali inapaswa kupongezwa mmeweza pamoja na msukosuko wa uchumi kuwa na fedha ya kuendelea kugharamia miradi yetu mikubwa kama barabara na hasa barabara yetu ya kutoka, Kagoma-Muleba-Kasindaga-Biharamuro hadi Rusahunga, inaendelea vizuri sana baada ya kubadilisha mkandarasi ambaye alikuwa hafanyi kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye eneo la mradi wa Umwagiliaji Kata ya Ikondo ambayo imegawanywa sasa eneo hilo ambalo linafanyika mradi wa umwagiliaji ni Kata mpya ya Buhangaza, utekelezaji wa mradi huo wa umwagiliaji ambao ni muhimu kwetu na ambao ndiyo wa kwanza umesuasua sana na haujaanza ingawa Wataalam wapo. Kwa hiyo, nashauri Serikali iongeze kasi katika vipaumbele ambavyo inaviainisha na pesa zinapotengwa ihakikishe utekelezaji unakwenda kwa kasi kwani kasi hairidhishi katika huo mradi wa umwagiliaji ambao ungenufaisha vijana wengi ambao hawana ajira

katika Kata ya Ikondo na Kata mpya ya Buhangaza kwa kuanzia na uwezekano wa kuweza kupata mabwawa ya umwagiliaji kwa Tarafa ya Nshamba, Muleba na Kimwani upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mito inayotiririka mwaka mzima na inaelekea Ziwa Victoria. Lakini maeneo ya kulima ni madogo ambayo yangetuwezesha hata kuvuna mara tatu katika zao la maharage. Kwa hiyo, nimefurahi sana kuona kwamba mtajenga miundombinu ya mabwawa kwa ajili ya umwagiliaji Muleba ya kusini mtupatie kipaumbele na hapa napenda kusema kuwa kwa eneo la Muleba kusini sisi tuko kwenye hatari kubwa sana kwa sababu sasa hivi tumepata shambulio la gonjwa hatari Wataalam wameliita Mnyauko. Kuna kirusi kinakula migomba yetu, migomba inaoza na inanuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wataalam wametoka Uganda na wengine nimekutana nao wanatoka Kenya wakishirikiana na Wataalam wetu kutoka Maruku wamezunguka kwenye maeneo yetu kuangalia tatizo hilo. Wameangalia wakaondoka wakatuahidi kwamba kuna chanjo ya kuzuia gonjwa hilo la kirusi na sisi Muleba kusini tunategemea migomba kwa ajili ya chakula. Tunakula ndizi na tunategemea ndizi hizo hizo kama zao la biashara. Tunauza ndizi Shinyanga,Mwanza watu wanaoishi Kahama huko wanajua ndizi zetu ni tamu sana na utamu wake hauna mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachoomba Mheshimiwa Waziri Mkuu nimeshaongea na Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Ushirika, amesema atakwenda. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu amwezeshe Waziri wa Kilimo aende haraka sana kwa sababu hajaondoka tangu Bunge hili limeanza namwona humuhumu ndani. Nasema kule ndizi zinakwisha na huyu ni mtani wangu Mheshimiwa Wasira, anadhani ni mzaha. Tutakufa kwa sababu Serikali haiwezi kulisha watu wa Muleba kusini migomba ikioza yote. Mheshimiwa Wasira nakuomba uondoke na ukichelewa nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akuagize uondoke haraka sana kwa sababu hili ni jambo la kutisha, anaweza akadhani natania Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipozungumza mambo ya malaria huko Muleba kwamba watoto wanakufa kuna watu humu walidhani nafanya mzaha. Watoto wakafa kweli lakini Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipomtuma Mheshimiwa Mwakyusa, nikaenda naye akashuhudia watoto wanavyokufa kwa malaria, hatua zimechukuliwa, wakadhibiti, malaria imekoma, watoto hawafi, vitanda ni vitupu, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali nzima ya Awamu ya Nne, ni sikivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Stephen Wasira sitaki utani aende Muleba, tutakufa kwelikweli naomba mnisaidie huu Mnyauko utatuua. Ndiyo maana hata na nguvu ya kujadili bajeti hii sina ninaishia kwenye Mnyauko na Uchaguzi na njaa haviendi pamoja. Kuna mwananchi mmoja Kata ya Kishanda migomba yote imeoza amepanda tumbaku katikati ya kijiji na tumbaku hailiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni hasira kwa sababu hata haina soko kwetu sasa hili ni jambo ambalo si la mzaha. Mheshimiwa Wasira kama hana nauli, bajeti ipitishwe haraka sana, aondoke, akaangalie matatizo hayo, amletee Mheshimiwa Waziri

Mkuu amweleze Mheshimiwa Rais ambaye maamuzi yake ni ya msingi sana kwenye mambo mazito kama haya ili tuondokane na Mnyauko.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho msiogope kukopa. Siungi mkono uamuzi wa Serikali wa kupunguza dhamana kwa Mashirika ya Umma kukopa. Kopeni tujenge reli, kopeni tujenge barabara. Hii ya kusema sijui deni lisilotekelezeka dunia nzima inakopa, Wamarekani walikuwa wanadaiwa trilioni tatu *dollar* za Kimarekani na nchi ya Uchina. Sasa sisi tunaogopa kukopa! Greece karibu wafilisike wameokolewa, Spain wako kwenye *line* ya kusaidiwa. Sisi tukope ili tujenge miundombinu. Ni nchi gani inasomba mafuta kwa gari wakati kuna reli kila ninapopita kwenda Muleba kule matrela, matrela tunaharibu hata barabara zetu. Mizigo mizito inasafirishwa kwa reli na ipo tukope. Tukope *NSSF, PPF, Government Pension Funds* mnaona miujiza iliyofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma, nayo ni ujasiri wa Mheshimiwa Rais na Serikali yake, huo ndiyo mfano mzuri wa kutumia rasilimali za ndani hatukukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo Kikuu kile cha Dodoma hakuna Afrika nzima kwa uzuri na kwa ukubwa na ni cha kisasa kabisa. Vinginevyo tutakaa tunaogopa kukopa hatutafanya kitu na Wabunge tumekopa sana si mnajua? Mimi bila kukopa nisingekuwa na baadhi ya mali nilizonazo, wewe utaiba?

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa kunisikiliza, nakwenda kushughulikia Mnyauko.

**NAIBU SPIKA:** Na unaunga mkono hoja isipokuwa Wasira aende huko mahali. Mheshimiwa Thomas Mwag'onda atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe na atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mungai.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kukupongeza kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwenye hii keki ya Taifa kwa maana ya bajeti kuu ya Taifa. Nashukuru pia kuwa kwamba Kaka yangu Mwakyembe ndiyo atakuwa anafuatia kunisukuma kuchangia katika uchangiaji huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wabunge wenzangu wote kwa ruhusa yako naomba nichukue nafasi hii kuwatakia heri katika hicho kinachokuja hapa karibuni hasa kwa wale wa CCM kwenye *nomination process.* Naomba kuwaambia kuwa unapokuwa Mbunge ujue kuna kuchaguliwa ama kutochaguliwa ni mambo ya kawaida. Kwa hiyo, naomba yale matumbo yanavyokuwa joto basi muweze kupunguza na kuweza kuwakilisha wananchi mpaka mwisho wa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi dakika kumi zinanipa taabu kidogo, sasa sijui nitakwenda hovyo ama nitakwenda sawa lakini nitajitahidi kadri ya uwezo wangu niweze kuingiza yale ambayo nilikuwa nimedhamiria. Nianze kwanza kwa kukipongeza Chama cha Mapinduzi hasa kwa kuamua kuwa na sera ya kuwezesha wananchi wake wa

Tanzania, kimekuwa na sera ya kuwa *SACCOS*, kumejitokeza vyombo mbalimbali kama VIKOBA na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa maana suala zima la uwezeshaji limefanyiwa kazi lakini nina mawazo yangu kidogo tofauti hasa baada ya kuipitia bajeti ambayo imesomwa na Waziri wa Fedha. Serikali katika bajeti ya mwaka 2009 kwenda 2010 ilidhamiria kukopa kiasi cha shiligi bilioni 500 na ushee hivi ili kuhakikisha kuwa wananchi wanakuwa na uwezekano wa kukopesheka fedha hizi, lakini zilizopatikana ni kwenye bilioni 150 na kitu.

Sasa nataka niseme kweli tuna Kilimo Kwanza kwa maana ya kuweka msisitizo kwenye kilimo, tumeongelea masuala ya miundombinu barabara na kadhalika lakini huko barabarani tukumbuke Serikali ya CCM tumechaguliwa kwenye msingi wa Maisha Bora kwa Kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mawazo yangu, nadhani kuna haja ya kui–*double* kuifanya ikawa mara mbili, kwa nini tusikope trilioni moja? Kwa sababu wananchi hawa sio kwamba wanachukua bure watakuwa wakilipa riba na kuhakikisha kwamba wanarudisha kwani mzunguko wa pesa utakuwepo. Mwananchi wa Tanzania atakapoweza kupata milo mitatu ndiyo ataona kweli tumemtendea haki, hii itatupa unafuu sana kwenye majukwaa yetu ya kisiasa na hata katika kazi zetu mbalimbali kama Wabunge na kama viongozi wa Serikali, naomba sana Serikali iliangalie hili upya wakati tunavyofanya hivi vipaumbele *prioritisation* mambo yale muhimu kwa nchi yetu tuyaangalie, tunapomgusa mwananchi mojakwa moja tunajijengea uhalali mzuri sana wa kuweza kuiongoza nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Rais Jakaya Mrisho Kikwete alikuja kwenye ziara nadhani mwaka jana kule Mkoa wa Mbeya. Alikuwa anafungua samani tawi la *CRDB* pale Mbozi nadhani *NMB* nao walikuwepo pale *Tanzania Postal Bank* nao walikuwepo sasa ikaonekana palikuwa kidogo na utata fedha za mkopo zilizotolewa kwa ajili ya kukopesha wananchi ikaonekana fedha zilitolewa, lakini katika kurudia kuwakopesha tena zile fedha hazikufika kwa wananchi. Naomba niwashauri Serikali katika umuhimu wa kufuatilia hilo na kuona kwamba wananchi wanaendelea kupata zile fedha walizoahidiwa na Serikali naona muda unakuwa mdogo lakini ngoja nijitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni matumizi ya Serikali, juzi nilikuwa nimekaa na wenzangu kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama mojawapo ya jambo nililoongelea ilikuwa ni mshangao wangu. Waziri Mkuu wakati alipokuwa *White Sands Hotel* pale mwaka jana au mwaka juzi mtanisaidia kidogo kwa hilo, alitoa maelekezo na maelekezo haya yangeweza kutusaidia sana, alitoa maelekezo kuwa haya magari aina ya mashangigi tuachane nayo kimanunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni kuwa wako Wabunge humu ndani ambao walijaliwa katika fedha za mkopo wa magari kununua magari mapya kabisa, leo hii ukiangalia magari yao baada ya miaka mitano yanafanya kazi vizuri kabisa, suala langu ninajiuliza kuwa iko haja kweli kila baada ya miaka miwili, mitatu tuwape magari

mapya wenzetu wa Serikalini? *Five years* nina hakika kabisa gari litakuwa bado linaendesheka vizuri kwa nini tufanye matumizi yasiyo ya lazima? Jamani ninachoomba uchungu wetu tuuzidishe kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nilitaka niongelee fedha za Mfuko wa Jimbo, hapa naomba nilie kilio cha Madiwani siyo kwa ajili ya Uchaguzi lakini kwa hali halisia. Wabunge sisi wale wa Majimbo sisi wa kuteuliwa hatukupata lakini *Inshalah* labda na sisi tutaingia huko siku moja. Kilichotokea wale Madiwani wanalipwa ofisini nadhani na viposhoposho kidogo lakini wale ndiyo kila siku wanakaa na kugongewa na wananchi milangoni kwa shida zao sasa nilikuwa nadhani kuwa angalau kwa bajeti ijayo hata kama hatupo kuwa zile fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri basi angalau vifungu hivi kwa udogo wake, Madiwani nao wapate ili nao waweze kuhudumia wananchi na watatusaidia hata sisi Wabunge kupungunza mzigo kubaki peke yetu, nadhani labda hili tulifikirie pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kwenda haraka kidogo ili kuingiza hizi *point* mbili tatu nilizopania ziingie, ni mkakati mzima wa ukamilishaji wa fedha za bajeti yetu za Wizara mbalimbali. Kamati inayotoka labda siyo vizuri sana kuzungumzia mambo yake maana ni Kamati ina utofauti kidogo ni ya Ulinzi na Usalama, lakini nilichogundua ni kwamba hili jambo linagusa Wizara nyingi sana, unakuta kwa mfano, iko Wizara moja tulikaa kwenye kikao fulani hivi tukakuta Wizara ya Fedha inadhani imetoa fedha kwa 96.4% lakini walichosahau ni kuwa zile fedha zilitumika kwa matumizi mengine ya Serikali nje ya Wizara, kwa hiyo, kuna kitu, kama hakuna uelewano na unakuta mpaka tunamaliza mwaka wa fedha baadhi ya fedha hizi Wizara nyingine hazijapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inaweza ikafikia tukaona Mawaziri wetu hawafanyi kazi vizuri lakini kwa ukweli mkakati muhimu unatakiwa uandaliwe kwa ajili ya Wizara zote kuhakikisha kuwa kuna ukamilishaji wa fedha tunazoziandaa kwa ajili ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyanzo vya mapato, mimi nimekuwa nachanganyikiwa kidogo hasa baada ya bajeti yetu kupunguzwa mwaka huu na hawa Waheshimiwa wa Ulaya kwa bilioni mia mbili na sabini na sisi imetubidi tulazimike kukopa, nchi yetu inaongozwa kwa msingi wa ujamaa na kujitegemea, hilo la ujamaa nisilijadili sana lakini lile la kujitegemea nadhani ni la muhimu sana, inakuwaje ndani ya miaka 40 bado hatuwezi kujitegemea?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo, kwa hotuba nzuri ya bajeti kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia masuala machache kulingana na muda wa kuchangia ulivyo mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri imekiri pamoja na mambo mengine kuwa mapato yetu ya ndani hayawiani na mahitaji makubwa ya nchi na vile vile hotuba inapendekeza hatua kadhaa zichukuliwe ili kuweza kurekebisha hali hiyo, mimi nitaongelea tu hatua mbili alizozitaja Mheshimiwa Waziri kati ya hatua kumi na mbili alizozipendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuziba mianya ya ukwepaji kodi. Pamoja na mianya mingi ambayo Serikali inafikiria kuiziba, napendekeza Serikali ipitie mara kwa mara au kila mwaka orodha ya wafanyabiashara wenye rekodi ya utii wa taratibu na sheria ambao mizigo yao ikifika bandarini haikaguliwi, inapelekwa moja kwa moja kwenye *yard* zao, taasisi inayohusika ikiamini yale makaratasi kwamba kilichoandikwa hapo ndiyo kilichomo kwenye mizigo, utaratibu huu siyo mbaya ni mzuri kabisa ili kupunguza msongamano wa mizigo kwenye bandari yetu. Lakini kwa kuwa kwenye kila msafara wa mamba, kenge hawakosekani, ni muhimu sana kupitia hii orodha mara kwa mara ili kuweza kujua kenge aliyejipenyeza yupo wapi na ningeomba wakati Waziri anakuja kuhitimisha hoja yake hapa atueleze hao *compliant traders* ni wepi, ili sisi Wabunge tuweze kujua na wananchi waweze kusaidia, si ajabu huyu unayemwona ni *compliant* mwaka juzi sasa hivi amegeuka badala ya kuleta *raw material* anaingiza mashangingi humo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kudhibiti uchanganyaji wa *diesel* na mafuta ya taa, kitendo ambao kimeshamiri sana nchini kiasi cha kuwa moja ya sifa hasi tulizonazo Watanzania kwa nchi majirani zetu wa Afrika Mashariki zimeanza kuondoka, Mheshimiwa Dokta Mzeru ameliongelea suala hili kwa kirefu, kwa kweli tumefikia mahali ambapo hata viongozi wetu waandamizi wa nchi magari yanazimika katikati ya barabara kutokana na mchezo huo. Tatizo hapa ni unafuu wa bei ya mafuta, huo unafuu ndiyo unafanya hawa wafanyabiashara wanaopenda kutajirika haraka haraka wachanganye na *diesel* kuweza ku-*maximize profit* na kupata fedha nyingi zaidi. Ndiyo maana sasa hivi kama alivyosema Mheshimiwa Mzeru kuna gereji nyingi zimechipua kati ya Dar es Salaam mpaka Chalinze kwa ajili ya kazi hiyo, matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa mara kwa mara wa magari na vile vile kuongeza gharama kwa wananchi pale ambapo wenye magari wanaongeza ada ya kusafirisha mizigo na vile vile kwa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nia ya Serikali mwanzoni ilikuwa nzuri tu kwamba tuwape unafuu wananchi wetu ambao hawana umeme waweze kutumia mafuta ya taa kwa ajili ya kupikia na kwa ajili ya usiku. Lakini sasa hivi inaonekana hiyo faida kwa kweli haiendi kwa wananchi wetu, ni kidogo sana, faida kubwa inakwenda kwa hawa Mafisadi wachache ambao wanatumia hiyo nishati ya mafuta ya taa kuchanganya

na *diesel*. Ninapenda kusema kwamba katika hili hakuna *shortcut,* tumeshaaibika kama nchi, mimi naomba tuondoe huo unafuu wa mafuta ya taa, ndiyo tutamaliza tatizo hili. Hatuwasaidii wananchi wetu, tunajidanganya hapa, kama tunahitaji kuwasaidia Watanzania zipo njia nyingi, tuwaondolee michango mbalimbali ya shule na kadhalika, lakini siyo mafuta ya taa ambayo badala ya kuwasaidia wao, yanatumiwa na mafisadi wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhishwa na vipaumbele vyote vilivyowekwa kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011. Tatizo langu mimi ni kwamba, hivi tutaanza utekelezaji na kipaumbele kipi? Kwa mfano, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tuna ukarabati mkubwa na urekebishaji, upanuzi wa viwanja vyetu vya ndege, nina wasiwasi kwamba tutaanza na ukarabati kwa mfano wa uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, tukifanya hivyo kabla ya kuboresha na kupanua, kukarabati barabara za Dar es Salaam tutakuwa tunajiletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapokea ndege nne au tano tu mpaka sita kwa siku katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere, lakini pamoja na hizo ndege chache, kutoka uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kwenda sehemu yoyote ya Jiji la Dar es Salaam, ni sawa na usafiri kwenda Johannesburg kwa ndege, kwenda Addis Ababa, halafu leo upanue uwanja wa ndege ziongezeke, mategemeo ni nini? Itakuwa ni *disaster* badala ya kuisaidia nchi. Mimi nadhani uimarishaji wa miundombinu ya barabara katika Jiji la Da es Salaam uwe kipaumbele namba moja, kwa kuwa Dar es Salaam siyo tu ni kitovu cha biashara vile vile ni kitovu cha uzalishaji wa viwanda, kitovu cha mawasiliano na kitovu cha usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na bajeti ya kilimo ambayo imeongezeka na mimi najua safari hii hata mbolea ya ruzuku kwa wananchi itaongezeka, nasikitika Kyela safari hii tumepata mbolea nyingi ya ruzuku lakini wakulima wengi hukosa hiyo mbolea kutokana na ubadhirifu na njia za panya ambazo zimetumika kutokana na utaratibu mbovu tuliouanzisha kama Serikali. Ninaiomba Serikali safari hii tuwahusishe viongozi wa wananchi wanaowajibika moja kwa moja kwa wananchi, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wahusike katika mchakato huu siyo watendaji ambao wanawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, ningeomba ifanyike hiyo ama sivyo ongezeko la mbolea ya ruzuku haitatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema uchumi wa kisasa wenye fursa ya kukua, unahitaji maamuzi *timely* yaani maamuzi katika muda muafaka, Mheshimiwa Lucy Mayenga ameliongelea sana hilo suala. Siyo tu maamuzi upande wa Serikali lakini pia upande wa Mahakama, huwezi kuwa na uchumi unaokua pale ambapo kesi zinakaa Mahakamani mwaka mmoja, miwili na kuendelea, zinashindwa kuamuliwa na huwezi kuwa na uchumi wenye fursa ya kukua pale ambapo maamuzi Serikalini yanakwamakwama, nitatoa mfano mmoja mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, Mkoa wa Mbeya ulikumbwa na giza kubwa kwa sababu transfoma yake kubwa iliharibika, ikalazimika *TANESCO* watumie ubunifu kwenda kuchukua transfoma Mgololo, ndiyo ambayo inatumika leo lakini

Serikali yetu sikivu imenunua transfoma mpya kwa ajili ya Mkoa wa Mbeya. Hiyo transfoma iko juu ya gari ikisubiri kusafirishwa kwenda Mbeya kwa miezi mitatu sasa kwa ajili tu ya Afisa mmoja Wizara ya Miundombinu hataki iende kule na sisi tunamwangalia, hivi mpaka Waziri Mkuu aingilie suala dogo kama hilo? Tukiwawajibisha, ndiyo wanakimbilia kuanzisha magazeti, kututukana ovyo ovyo hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba mimi ni kiongozi na watu wa Wilaya ya Kyela, ni waelewa, hayo magazeti yanatumika kufungia vitumbua vya mchele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuongelea suala la sukari ya Malawi. Mkoa wa Mbeya wote, kuanzia viongozi wa kisiasa wa juu mpaka vyombo vya usalama, wanatumia sukari ya magendo, Mheshimiwa Mkullo lielewe hilo. Sukari imekuwa ya magendo zaidi ya miaka kumi, vijana wangu Kyela wanaosomba hiyo sukari kwa baiskeli kutoka Malawi, wanakamatwa kila siku na *TRA*, mimi ningeomba ukija hapa, nimesema naunga mkono hoja mapema lakini naweza kubadilika, nakuomba ukija hapa uniambie toka mmeanza kuwakamata vijana wangu Kyela, wanaosomba sukari mifuko miwili, mitatu kutoka Malawi wanakamatwa na wanachukuliwa hiyo sukari yao, Serikali imepata kiasi gani cha pesa, naomba nielezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama si hivyo, naomba leo utoe uamuzi, nimeshalileta suala hili kwa Mawaziri waliopita wameshindwa kuliamua, maamuzi madogo madogo haya, ruhusu Sukari ya Malawi iingie Mkoa wa Mbeya, weka viwango na Serikali ipate kidogo ushuru. Vijana wangu unaweza ukawaambia walipe shilingi elfu tano kwa mwaka, wanaouza kwa baiskeli watakuwa *compliant,* watalipa. Tunakaa na hili suala, ninyi Mawaziri wote mmekuja Kyela hata Waziri Mkuu ananiangalia, ile chai tunayowapa pale ni sukari ya magendo, ninawahakikishia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini tuishi kwa unafiki huu badala ya kulihalalisha suala hili, tuhalalishe Serikali ipate kidogo, wananchi wangu waishi kwa starehe, vijana wangu wanakamatwa kila siku. Vijana wangu wanavusha sukari katika mazingira magumu, *TRA* wapo pale na ndiyo maana ya kuwahamisha *TRA* na Polisi Wilayani Kyela, ni maisha magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini ya transfoma, hebu pelekeni aah! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Joseph Mungai, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya bajeti. Napenda pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Wilaya ya Mufindi ambao wameniwezesha kuwa Mjumbe wa Bunge hili na kushiriki katika mijadala ya aina hii, huu ukiwa ni

mwaka wangu wa 35 katika Bunge hili, nikijumlisha na ile miwili ya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa wakati ule tukiwa *Ex-official MP's*, basi mwaka huu natimiza karibu miaka 37 kama Mjumbe wa Bunge hili na inaelekea kwa ridhaa ya wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, nitaendelea kuwemo katika Bunge linalokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia kwangu, naomba niseme tangu mwanzo kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha, kwa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa utekelezaji wa Ilani, Ilani imetekelezwa kwa mafanikio makubwa sana. Nami ninapenda kujikita katika maeneo mawili ambayo ni miundombinu na upanuaji wa elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na miundombinu. Serikali ya Awamu ya Nne, imeendeleza kwa ufanisi mkubwa kazi iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu, barabara zinazidi kutengenezwa na kuwa bora zaidi kwa kuwekwa lami na nchi yetu inazidi kuunganika vizuri zaidi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkoa wa Iringa, Serikali ya Awamu ya Tatu, barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Iringa, ilitengeneza eneo korofi la Kitonga kilomita tisa, sisi wananchi wa Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Mbeya, ile sehemu ya barabara hiyo (Kitonga), ni kama lile daraja la Mto Rufiji, bila kutengeneza eneo hilo basi tutakuwa tumetengana kabisa na Makao Makuu ya Nchi ya sasa yaliyopo Dar es Salaam. Lakini Serikali ya Awamu ya Nne, imeendelea kuitengeneza barabara hiyo siyo pale Kitonga tu, mbele kidogo ya Mikumi hadi mbele kidogo ya Mji wa Iringa barabara ile inatengenezwa kwa kutandikwa upya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa, napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kuitengeneza barabara hiyo. Ushauri wangu ni kwamba, barabara hiyo ingeendelezwa kabla huyu Mkandarasi hajamaliza *contract* yake, ingeendelezwa mpaka Mikumi ili iunganike vizuri na ile sehemu ya Mikumi - Morogoro iliyotengenezwa vizuri, kisibaki kile kiraka pale.  Lakini pia ninashauri barabara hii badala ya kuishia mbele kidogo ya Mji wa Iringa, Kijiji kinachoitwa Gwachanya, Njiapanda ya kwenda Tosamaganga, ninashauri barabara hii ingeendelezwa kutengenezwa mpaka Mbeya hadi Tunduma, hapo faida za kiuchumi za barabara hii zitakuwa ni kubwa zaidi. Tungeiomba Serikali kwamba Mkandarasi huyu ambaye anaonekana anafanya kazi nzuri basi wangefanya naye mazungumzo ili aweze kuiendeleza barabara hii katika awamu ya kwanza ifike angalau Makambako lakini ifike Mbeya hadi Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya pili ambayo wananchi wa Mkoa wa Iringa tumefurahi sana kuona Serikali imekwishakamilisha upatikanaji wa fedha za barabara hiyo ni barabara inayounganisha Iringa na Dodoma na pia kutoka Dodoma kwenda Babati. Huu ni uamuzi mzuri na naipongeza sana Serikali kwa kufanya jitihada kupata fedha ili barabara hii itengenezwe. Barabara hii ni sehemu ya barabara kuu ya Kaskazini inayojulikana kama '*Great North Road'* inayotoka *Cape Town* mpaka Cairo. Barabara hii, ina umuhimu mkubwa sana kwa nchi yetu, inatuunganisha na masoko makubwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, masoko makubwa ya nchi za *SADC* na pia masoko

makubwa unapoelekea kule Cairo ya nchi za *COMESA*. Barabara hii ikiunganishwa vizuri, nchi yetu itaweza kufanya biashara kubwa na masoko hayo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Serikali kwa maandalizi ambayo imekwishayafanya kutengeneza barabara ya kutoka Rujewa, Madibira mpaka Kinyarambo, tumeona harakati nyingi za kukamilisha makisio ingawaje kazi haijaanza. Waziri wa Miundombinu alifika Wilayani kwetu, akatuhakikishia kwamba barabara hii itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara hizi, napenda kuihakikishia Serikali kwamba wananchi wa Mkoa wa Iringa, kwa mara nyingine tena, tutahakikisha ushindi mkubwa kwa CCM kwa asilimia mia moja kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa elimu, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kupanua Elimu ya Msingi, Sekondari, Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Huu ni utekelezaji mzuri sana wa Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya CCM, imetamkwa wazi kwamba elimu itapanuliwa katika ngazi ya elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya chuo kikuu. Nilimsikia Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Zitto Kabwe akisema *University of Dodoma* ni sera ya CHADEMA, mimi nadhani hapa alijiingiza kufafanua msaafu usio wake, Ilani ya CCM, ni msaafu wa CCM na katika Ilani, imetamkwa wazi kupanua elimu ya Chuo Kikuu na ukisema kupanua elimu ya Chuo Kikuu sasa suala la wapi…

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia saa, naona bado nina *time* kidogo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka ieleweke kwamba katika Ilani hutamki kila *details*, suala la Chuo Kikuu cha Dodoma linaingia kwenye *detail*, napenda kutoa angalizo kwamba tuangalie masuala ya ufanisi katika elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda nilichangie kwa kifupi kabisa ni hili suala zima la kukopa mikopo ya ndani ya kibiashara kwa kiwango cha bilioni elfu mbili. Hii inaweza kuleta athari kubwa sana katika uchumi, muda hauniruhusu kuingia katika kuzitamka hizo athari lakini napenda tu nitumie nafasi hii kuishauri Serikali, iwe kama mtu wa kawaida unapokuwa na mahitaji ya fedha, cha kwanza unachoanza siyo kukimbilia kukopa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante, ni kengele ya pili sasa.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi, namalizia kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nami nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwepo mahali hapa wakati huu lakini pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi, walionichagua miaka mitano iliyopita, nikaweza kuwepo mahali hapa, nami naamini nimekuwa nikiwasemea na ninaendelea kuwawakilisha na ninaamini wamekuwa na imani na kazi ambazo tumekuwa tukifanya kwa ushirikiano mkubwa katika Jimbo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wake na maofisa wote wa Wizara hiyo, ninawapongeza kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea hapa, mimi naamini bajeti hii itatuvusha katika mwaka huu wa 2010 mpaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya pamoja na Serikali yake. Nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya na ambayo anaendelea kuifanya na ambayo naamini Watanzania wote watajumuika pamoja kumpa kura nyingi za kumvusha na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine tena. Mimi namwomba Mwenyezi Mungu awajalie Wabunge wote walioko hapa, wanapokwenda Majimboni, wote wakabarikiwe na wote warudi salama na Mungu atawajalia mrudi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme mambo machache. Kuna kitu kimoja nilikiona nikasema lazima nikiseme, nacho ni *balance* kati ya *recurrent expenditure* na *revenue* ya mapato yetu ya nchi hii. Ukiangalia pale *recurrent expenditure* yenyewe iko kwenye shilingi *7.8 million* lakini mapato ni shilingi *6 trillion*. Sasa ukichukua hiyo, ukalinganisha maana yake ni kwamba 1.8 ni misaada itokayo nje. Sasa hiyo mategemeo yake ni kwamba wahisani watatupa fedha hizo kwa wakati lakini kuna tatizo kubwa ambalo wanaliita *"predictability"* kwamba kama hii misaada haikuja kwa wakati, ni dhahiri mipango yote uliyopanga na hata matumizi yote uliyopanga kufanyika kwa kipindi hicho, unaweza usifanikiwe kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili ni jambo ambalo lazima tuliangalie sana. Hii habari ya misaada, ni jambo kubwa. Sasa hivi ulimwengu mzima wanazungumza habari ya *aid transparency, aid coherence* na mambo mengine, jinsi unavyoweza kulinganisha na kurekebisha utaratibu wa misaada na jinsi tunavyotakiwa kuonyesha kwamba hii misaada tunaitumia vizuri kwa kazi za maendeleo. Tanzania ni mfano mzuri wa nchi ambayo imekuwa ikipata misaada mingi na sisi kwa kweli tumekuwa tukijitahidi kuitumia vizuri. Nawapongeza sana Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini misaada maana yake nini? Misaada maana yake ni hali kubwa ya utegemezi. Utegemezi huu sisi hautusaidii sana kwa maana ya kufika mahali tujitegemee. Kama tunaweza kutumia fedha hizi, zikatuondoa hatua moja, mwaka kesho tukaja tukawaambia Watanzania kwamba sasa tulipofika tumepunguza asilimia 20 ya kujitegemea na mwaka kesho tunaendelea kupunguza, lakini *level* ya utegemezi imeendelea kuwa pale pale, hii ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania tuna rasilimali nyingi, tuna kilimo kizuri, tuna misitu, wanyama wengi, mapato yetu yangeweza kuendelezwa vizuri sana. Nafikiri Watanzania hatuhitaji kuelezwa juu ya rasilimali ambazo tunazo, tunayo madini mengi, misitu mingi, tuna mabonde mengi, kwa mfano mabonde ya Kigoma peke yake tungeweza kuyatumia vizuri, yangelisha nusu ya nchi hii na yangelisha na Burundi yote. Tunachohitaji ni utaratibu mzuri tu ambao utatuwezesha kutumia rasilimali nyingi tulizonazo. Mabonde haya, ni muhimu yakatumika na ni muhimu yakaonekana yana faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini na nakubaliana na wale rafiki zangu ambao wamekuwa wanazungumza kwamba rasilimali zingine nchini ni *sleeping giants*, nilikuwa nafanya kazi na *Canadian International Development Agency* wakati fulani, nikaenda Basuto, kwa kweli nilishangaa sana kwamba *infrastructure* ambayo ingetufanya sisi tujitegemee kwa kulima ngano, leo hii inakufa na katika vitu vilivyokatisha tamaa Ubalozi wa Canada ni *infrastructure* ile kuachwa hivi hivi. Lakini taratibu na misaada ambayo tumepata iko mingi ambapo tungeiendeleza ingeweza kutusaidia sana. Hivi kwa nini hatutaki kujitegemea katika kilimo cha ngano wakati tuna *import* ngano nyingi sana na tungeachana na ngano ya kutoka nje. Maana ngano ingeweza kutusaidia sana. Yako mambo mengine hatuhitaji mtu kutoka nje aje kutufundisha, ni mambo ambayo sisi wenyewe tunayafanya na tumeyafanya toka utoto wetu wengine tunayaona tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu si kilimo kikubwa kinahitaji *transformation*. Sasa tunazungumza habari ya *power tillers.* Kwa mfano, Kigoma tuliambiwa *power tillers* itauzwa kwa shilingi milioni nne mpaka sita lakini inafikia shilingi milioni tisa mpaka 10, hizi gharama zimetoka wapi? Naomba Waziri atakapokuwa ana-*wind up* pengine nielezwe tu hizi gharama nyingine kama ni gharama za Halmashauri kushughulikia maana zimekuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitoe tu tafadhali kwamba katika utaratibu wa bajeti yetu hii, kuna mambo nayaona ni makubwa sana, moja ni hilo la uchaguzi ambao *obviously* litachukua gharama kubwa lakini la pili, ni hilo la Vitambulisho vya Watanzania ambavyo tunavihitaji sana lakini la tatu ni mishahara kupanda. Katika uchumi wa kawaida, ukifanya yote haya kwa pamoja lazima utapata tatizo. Kwa hiyo, hii ni *caution* tu natoa haya mambo matatu yana *pressure* au *very high demand on public expenditure*, yote haya yanafanywa katika bajeti ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, lazima tukubali kwamba baadhi ya matumizi mengine itabidi *at some point* yaweze kusitishwa, haitakwenda kama ambavyo inafikiriwa. *Of course,* jinsi inavyo-*feed back* kwenye *economy,* matatizo yapo, hatutayakwepa, tuwe tayari kwenda kuhakikisha kwamba *as much as borrowing from the banking system* inakuwepo liko tatizo ambalo litajitokeza na

hilo tatizo mimi naamini Wizara ya Fedha ina watalaam wazuri na sasa Wizara ya Mipango, wataalam hawa watasaidiana kuangalia na kuhakikisha kwamba *process* nzima hii haiwi *inflationary*. Nalisema hili kwa kuelewa kwamba hayo yote lazima yatakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali yetu na hasa tunapofikiria bajeti nzima kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni hili ambalo linawahusu wananchi wetu kule vijijini. Sehemu nyingi kuna migogoro ya mipaka na hiyo ninaomba Wizara inayohusika iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mola, kwa kunifikisha salama na kupata nafasi hii ya kuchangia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwashukuru wapiga kura wangu wote wa Mji Mkongwe, kwa kuonesha imani kubwa sana juu yangu kwamba nilifanya na naendelea kufanya kazi zao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na Jimboni kwangu na kwa kuridhia tena niwe mgombea na kilichobakia sasa hivi, kama itawezekana hata niapishwe kabisa kabla ya huo uchaguzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nizungumzie kidogo kuhusu namna gani tunaweza tukawasaidia wavuvi. Sikatai bajeti kuelekezwa kwenye kilimo, ndiyo uti wa mgongo. Asilimia kubwa ya wananchi wetu wanazalisha chakula kwa ajili yao na kwa ajili ya ziada ya kusafirisha nchi za nje lakini mvuvi kapewa nafasi gani? *Initial capital* ya mkulima inaweza ikaanzia hata shilingi 100,000 na kuendelea, inategemea na kilimo chake lakini mvuvi anahitaji si chini ya shilingi milioni 10 kuanzisha mradi wa uvuvi wa chini kabisa yaani kununua boti, kununua mashine kama Yamaha ambayo takribani inafika shilingi milioni 3.5, hizo ndizo fedha anazozihitaji. Hakuna *incentive* zozote zilizoonyeshwa na Serikali kwamba walau tupunguze viwango vya ushuru au kuondoa kabisa katika suala hili la uvuvi. Kutoka kijiji cha Moa mpaka Msimbati yaani kutoka Tanga ukanda wa mpaka Msimbati, Mkoa wa Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara karibu Wilaya tisa zina vijana wanaohitaji uvuvi wa kisasa ambao utawapa ajira wao na kuongeza mapato Serikalini. Sasa basi uvuvi haukwenda hapo tu hata kwenye maziwa yetu Mwanza, Rukwa, Mara, Kigoma, Bukoba, Mbeya mpaka Ruvuma ukiangalia Wilaya zote hizi si zaidi ya Wilaya 22 hivi, Serikali inashindwa nini hadi leo hii kutenga walau dola milioni 22 kwa mwaka mmoja tu kwa kila Wilaya wakapata dola milioni moja ili kuendeleza uvuvi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yamezungumzwa sana na Mheshimiwa Mudhihir, yamezungumzwa sana na Mheshimiwa Mongella, yamezunguzwa na Mheshimiwa Shah, yamezungumzwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, yamezungumzwa na Mheshimiwa Manju Msambya, kwa sababu uvuvi hauko kwenye maziwa tu. Leo tunasafarisha tani ngapi kutoka *Lake Victoria* kupeleka Ulaya? Hatuwezi kuingia bahari kuu kwa sababu gharama zake ni kubwa, vifaa vyake ni ghali, lakini hebu tuwawezeshe hawa wavuvi wadogo

wadogo kuwapatia misaada hii ya fedha wakaweza kujiendeleza, wakavua kwa faida yao wenyewe, wakaingiza mapato katika Serikali na ikawa ni sehemu ya kupata chakula kilichokuwa na *protein* katika ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema Serikali hii inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 350 kwa mwezi, hivi kutenga dola milioni 20 mpaka 22 kuwapatia vijana hawa, tunashindwa? Hizo ndizo ajira, hawa wakishajiajiri wenyewe, kikapatikana hicho kipato wataji-*engage* katika mambo mengine, watakuwa na vikundi vyao vya uvuvi. Tukiwaacha na kuwanyang'anya nyavu zao ndogo ili wasivue, wataanza kuingia kwenye mashamba ya watu waibe mahindi maana hawana la kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Tanzania tuna tabia ya kutaka makubwa, tuanze na mambo madogo. Hivi tunazalisha pamba nyingi sana lakini hatutengenezi vitambaa. Hadi leo hii miaka 40 ya uhuru nguo za Wanajeshi wetu, Polisi, Magereza zinaagizwa kutoka nchi za nje. Twende Syria tukaone wanafanya nini na pamba yao. Twende nchi ya *Egypt* tukaone wanafanya nini na pamba yao, tuwachukue wataalam kutoka India, Thailand, tunao vijana wa JKT washone nguo za Jeshi la Polisi ili tuhifadhi fedha za kigeni badala ya kuagiza nguo za Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania kutoka nchi za nje. Afrika Kusini wanajitegemea na nguo za vikosi vyao. *Egypt* na *Syria* wanajitegemea, kwa nini sisi tusijitegemee? Tubakie kuuza korosho ambazo hazijabanguliwa, tuuze pamba tusitengeneza viwanda vidogo, kwa nini? Tutapata ajira kwa ndugu zetu, ambao watatoa hizo nguo kwa ajili ya sare za Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, chekecheni muoni kiasi gani cha fedha za kigeni tunazoagiza nguo za Polisi, nguo za Wanajeshi, nguo za Magereza ili tutengeneze wenyewe. Pamba ipo Mwanza ya kutosha lakini tuna zile ndoto za nadharia, tuna *Uranium*, watu walishaanza ku-*predict* mambo ya ajabu ajabu, sijui umeme tutapata rahisi, *Uranium* ina matatizo, ina Sheria zake za Kimataifa, tunao watalaam wa *Uranium*, si zaidi ya wataalam 10, kiwanda kidogo tu cha kufua umeme wa *Uranium* kinahitaji wataalam 100 mpaka 150 waliobobea, leo utakwenda kuwachukua watu wa nchi za nje waje wasimamie kiwanda ambacho kinazalisha umeme kutokana na *Uranium*, hatuwezi, tuwaelimishe watu wetu kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalizungumzwa na Profesa Mkilaha mtaalam wa mambo ya Uranium, alizungumza hili kwamba hatuna watalaam wa kutosha, tuwaelimishe watu wetu kwanza, tuache *Uranium* na hayo mambo mengi tumeyavamia ndio tukafika hapa tulipo. Ilikuwa sisi hatuna haja ya dhahabu, hatuna haja ya *Uranium*, kilimo, ufugaji, utalii na bahari kuu, haki ya Mungu ingeendesha bajeti ya Tanzania na tukawa na fedha za ziada, lakini wapi tunabuni tu mambo. Watu wa kutaka ushauri wapo, hebu nendeni kwa Profesa Lipumba mkachukue ushauri, ni Mchumi mzuri tu anaweza akasaidia nchi yake hii. Kwa nini anachukuliwa na nchi za nje tusimtumie sisi? Muwahini Profesa Lipumba kabla hajafanya vitu vyake mwezi Oktoba *otherwise* tutakuja kuathirika hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania lazima ijikite katika masuala madogo madogo, makubwa tuyaweke kando kwanza. Tusafirishe bidhaa ambazo

zimetengenezwa, tuchukue matunda ambayo tunaweza tukasafirisha *juice*, korosho tupeleke ambazo zimebanguliwa, pamba tutengeneze nguo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Uandike kwa maandishi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba anaendelea kuniimarisha na naamini nitaendelea kuimarika baada ya tukio langu gumu na ninaamini ni hali ya kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda nichukue nafasi hii, kwanza kabisa na mimi kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Mwanza. Wanawake wa Mkoa wa Mwanza walinipenda, wakaniwezesha kuingia katika Bunge hili kwa muda wa miaka mitano na mimi ninawapenda hadi sasa na ninaamini wataendelea kunipenda ili niweze kuendelea kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza, kwa usafi wa Jiji hilo hadi leo tunaendelea kuongoza, kwa awamu tano mpaka sasa. Kwa kweli nasema hongereni sana Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango mzima wa bajeti, mara nyingi maeneo ya wafugaji huwa wala hayatajwi kabisa. Hata hivi sasa vipaumbele ni vizuri tu elimu, miundombinu, afya na vinginevyo lakini tusipozungumzia Wizara zingine hizi zinazobaki, inaonekana kama vile basi zinatupwa kapuni kabisa. Ukiona mwendelezo mzima katika matukio kwa mfano wenzetu wavuvi wanatetewa sana, wengine ambao wanaweza kutetewa ni wananchi ambao wanapata matukio kwa mfano ya mafuriko, wanabebwa haraka sana, lakini wafugaji jamani, ng'ombe wake wote wanakufa, anabaki mtupu lakini mbona Serikali huwa haishtuki haraka? Mimi sijaona Serikali inakwenda rasmi kwamba hawa ng'ombe wao wamekufa hawana hata mmoja, kwa mfano, Wamasai wanakosa maziwa, wanakosa nyama na ndio chakula chao. Sasa niwaombe wafugaji hebu mjikite kikwelikweli mtakapopata nafasi ya kuongelea ndani ya Wizara muone bajeti inazungumzia nini kuhusu wafugaji ambao hawana msaada kabisa na wengine wanafikia hata kupoteza maisha kwa sababu hajui tena ashike wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vyanzo vya mapato, mimi nimekuwa nachanganyikiwa kidogo hasa baada ya bajeti yetu kupunguzwa mwaka huu na hawa Waheshimiwa wa Ulaya kwa bilioni mia mbili na sabini na sisi imetubidi tulazimike kukopa, nchi yetu inaongozwa kwa msingi wa ujamaa na kujitegemea, hilo la ujamaa nisilijadili sana lakini lile la kujitegemea nadhani ni la muhimu sana, inakuwaje ndani ya miaka 40 bado hatuwezi kujitegemea?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. THOMAS A. MWANG'ONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nianze moja kwa moja kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mustafa Mkulo, kwa hotuba nzuri ya bajeti kwa mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia masuala machache kulingana na muda wa kuchangia ulivyo mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri imekiri pamoja na mambo mengine kuwa mapato yetu ya ndani hayawiani na mahitaji makubwa ya nchi na vile vile hotuba inapendekeza hatua kadhaa zichukuliwe ili kuweza kurekebisha hali hiyo, mimi nitaongelea tu hatua mbili alizozitaja Mheshimiwa Waziri kati ya hatua kumi na mbili alizozipendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuziba mianya ya ukwepaji kodi. Pamoja na mianya mingi ambayo Serikali inafikiria kuiziba, napendekeza Serikali ipitie mara kwa mara au kila mwaka orodha ya wafanyabiashara wenye rekodi ya utii wa taratibu na sheria ambao mizigo yao ikifika bandarini haikaguliwi, inapelekwa moja kwa moja kwenye *yard* zao, taasisi inayohusika ikiamini yale makaratasi kwamba kilichoandikwa hapo ndiyo kilichomo kwenye mizigo, utaratibu huu siyo mbaya ni mzuri kabisa ili kupunguza msongamano wa mizigo kwenye bandari yetu. Lakini kwa kuwa kwenye kila msafara wa mamba, kenge hawakosekani, ni muhimu sana kupitia hii orodha mara kwa mara ili kuweza kujua kenge aliyejipenyeza yupo wapi na ningeomba wakati Waziri anakuja kuhitimisha hoja yake hapa atueleze hao *compliant traders* ni wepi, ili sisi Wabunge tuweze kujua na wananchi waweze kusaidia, si ajabu huyu unayemwona ni *compliant* mwaka juzi sasa hivi amegeuka badala ya kuleta *raw material* anaingiza mashangingi humo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni kudhibiti uchanganyaji wa *diesel* na mafuta ya taa, kitendo ambao kimeshamiri sana nchini kiasi cha kuwa moja ya sifa hasi tulizonazo Watanzania kwa nchi majirani zetu wa Afrika Mashariki zimeanza kuondoka, Mheshimiwa Dokta Mzeru ameliongelea suala hili kwa kirefu, kwa kweli tumefikia mahali ambapo hata viongozi wetu waandamizi wa nchi magari yanazimika katikati ya barabara kutokana na mchezo huo. Tatizo hapa ni unafuu wa bei ya mafuta, huo unafuu ndiyo unafanya hawa wafanyabiashara wanaopenda kutajirika haraka haraka wachanganye na *diesel* kuweza ku-*maximize profit* na kupata fedha nyingi zaidi. Ndiyo maana sasa hivi kama alivyosema Mheshimiwa Mzeru kuna gereji nyingi zimechipua kati ya Dar es Salaam mpaka Chalinze kwa ajili ya kazi hiyo, matokeo yake ni uharibifu mkubwa wa mara kwa mara wa magari na vile vile kuongeza gharama kwa wananchi pale ambapo wenye magari wanaongeza ada ya kusafirisha mizigo na vile vile kwa abiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nia ya Serikali mwanzoni ilikuwa nzuri tu kwamba tuwape unafuu wananchi wetu ambao hawana umeme waweze kutumia mafuta ya taa kwa ajili ya kupikia na kwa ajili ya usiku. Lakini sasa hivi inaonekana hiyo faida kwa kweli haiendi kwa wananchi wetu, ni kidogo sana, faida kubwa inakwenda kwa hawa Mafisadi wachache ambao wanatumia hiyo nishati ya mafuta ya taa kuchanganya na *diesel*. Ninapenda kusema kwamba katika hili hakuna *shortcut*, tumeshaaibika kama nchi, mimi naomba tuondoe huo unafuu wa mafuta ya taa, ndiyo tutamaliza tatizo hili. Hatuwasaidii wananchi wetu, tunajidanganya hapa, kama tunahitaji kuwasaidia Watanzania zipo njia nyingi, tuwaondolee michango mbalimbali ya shule na kadhalika, lakini siyo mafuta ya taa ambayo badala ya kuwasaidia wao, yanatumiwa na mafisadi wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeridhishwa na vipaumbele vyote vilivyowekwa kwenye bajeti ya mwaka 2010/2011. Tatizo langu mimi ni kwamba, hivi tutaanza utekelezaji na kipaumbele kipi? Kwa mfano, nimesoma kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba tuna ukarabati mkubwa na urekebishaji, upanuzi wa viwanja vyetu vya ndege, nina wasiwasi kwamba tutaanza na ukarabati kwa mfano wa uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, tukifanya hivyo kabla ya kuboresha na kupanua, kukarabati barabara za Dar es Salaam tutakuwa tunajiletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunapokea ndege nne au tano tu mpaka sita kwa siku katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere, lakini pamoja na hizo ndege chache, kutoka uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam kwenda sehemu yoyote ya Jiji la Dar es Salaam, ni sawa na usafiri kwenda Johannesburg kwa ndege, kwenda Addis Ababa, halafu leo upanue uwanja wa ndege ziongezeke, mategemeo ni nini? Itakuwa ni *disaster* badala ya kuisaidia nchi. Mimi nadhani uimarishaji wa miundombinu ya barabara katika Jiji la Da es Salaam uwe kipaumbele namba moja, kwa kuwa Dar es Salaam siyo tu ni kitovu cha biashara vile vile ni kitovu cha uzalishaji wa viwanda, kitovu cha mawasiliano na kitovu cha usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa na bajeti ya kilimo ambayo imeongezeka na mimi najua safari hii hata mbolea ya ruzuku kwa wananchi itaongezeka, nasikitika Kyela safari hii tumepata mbolea nyingi ya ruzuku lakini wakulima wengi hukosa hiyo mbolea kutokana na ubadhirifu na njia za panya ambazo zimetumika kutokana na utaratibu mbovu tuliouanzisha kama Serikali. Ninaiomba Serikali safari hii tuwahusishe viongozi wa wananchi wanaowajibika moja kwa moja kwa wananchi, Wenyeviti wa Vijiji na Vitongoji wahusike katika mchakato huu siyo watendaji ambao wanawajibika kwa Mkurugenzi wa Halmashauri, ningeomba ifanyike hiyo ama sivyo ongezeko la mbolea ya ruzuku haitatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema uchumi wa kisasa wenye fursa ya kukua, unahitaji maamuzi *timely* yaani maamuzi katika muda muafaka, Mheshimiwa Lucy Mayenga ameliongelea sana hilo suala. Siyo tu maamuzi upande wa Serikali lakini pia upande wa Mahakama, huwezi kuwa na uchumi unaokua pale ambapo kesi zinakaa Mahakamani mwaka mmoja, miwili na kuendelea, zinashindwa kuamuliwa na huwezi

kuwa na uchumi wenye fursa ya kukua pale ambapo maamuzi Serikalini yanakwamakwama, nitatoa mfano mmoja mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana, Mkoa wa Mbeya ulikumbwa na giza kubwa kwa sababu transfoma yake kubwa iliharibika, ikalazimika *TANESCO* watumie ubunifu kwenda kuchukua transfoma Mgololo, ndiyo ambayo inatumika leo lakini Serikali yetu sikivu imenunua transfoma mpya kwa ajili ya Mkoa wa Mbeya. Hiyo transfoma iko juu ya gari ikisubiri kusafirishwa kwenda Mbeya kwa miezi mitatu sasa kwa ajili tu ya Afisa mmoja Wizara ya Miundombinu hataki iende kule na sisi tunamwangalia, hivi mpaka Waziri Mkuu aingilie suala dogo kama hilo? Tukiwawajibisha, ndiyo wanakimbilia kuanzisha magazeti, kututukana ovyo ovyo hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba mimi ni kiongozi na watu wa Wilaya ya Kyela, ni waelewa, hayo magazeti yanatumika kufungia vitumbua vya mchele. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuongelea suala la sukari ya Malawi. Mkoa wa Mbeya wote, kuanzia viongozi wa kisiasa wa juu mpaka vyombo vya usalama, wanatumia sukari ya magendo, Mheshimiwa Mkullo lielewe hilo. Sukari imekuwa ya magendo zaidi ya miaka kumi, vijana wangu Kyela wanaosomba hiyo sukari kwa baiskeli kutoka Malawi, wanakamatwa kila siku na *TRA*, mimi ningeomba ukija hapa, nimesema naunga mkono hoja mapema lakini naweza kubadilika, nakuomba ukija hapa uniambie toka mmeanza kuwakamata vijana wangu Kyela, wanaosomba sukari mifuko miwili, mitatu kutoka Malawi wanakamatwa na wanachukuliwa hiyo sukari yao, Serikali imepata kiasi gani cha pesa, naomba nielezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama si hivyo, naomba leo utoe uamuzi, nimeshalileta suala hili kwa Mawaziri waliopita wameshindwa kuliamua, maamuzi madogo madogo haya, ruhusu Sukari ya Malawi iingie Mkoa wa Mbeya, weka viwango na Serikali ipate kidogo ushuru. Vijana wangu unaweza ukawaambia walipe shilingi elfu tano kwa mwaka, wanaouza kwa baiskeli watakuwa *compliant,* watalipa. Tunakaa na hili suala, ninyi Mawaziri wote mmekuja Kyela hata Waziri Mkuu ananiangalia, ile chai tunayowapa pale ni sukari ya magendo, ninawahakikishia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa nini tuishi kwa unafiki huu badala ya kulihalalisha suala hili, tuhalalishe Serikali ipate kidogo, wananchi wangu waishi kwa starehe, vijana wangu wanakamatwa kila siku. Vijana wangu wanavusha sukari katika mazingira magumu, *TRA* wapo pale na ndiyo maana ya kuwahamisha *TRA* na Polisi Wilayani Kyela, ni maisha magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Lakini ya transfoma, hebu pelekeni aah! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitamwita Mheshimiwa Joseph Mungai, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya bajeti. Napenda pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru sana wananchi wenzangu wa Wilaya ya Mufindi ambao wameniwezesha kuwa Mjumbe wa Bunge hili na kushiriki katika mijadala ya aina hii, huu ukiwa ni mwaka wangu wa 35 katika Bunge hili, nikijumlisha na ile miwili ya kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa wakati ule tukiwa *Ex-official MP's*, basi mwaka huu natimiza karibu miaka 37 kama Mjumbe wa Bunge hili na inaelekea kwa ridhaa ya wananchi wa Jimbo la Mufindi Kaskazini, nitaendelea kuwemo katika Bunge linalokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia kwangu, naomba niseme tangu mwanzo kwamba naunga mkono hoja hii ya Waziri wa Fedha, kwa kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Nne, kwa utekelezaji wa Ilani, Ilani imetekelezwa kwa mafanikio makubwa sana. Nami ninapenda kujikita katika maeneo mawili ambayo ni miundombinu na upanuaji wa elimu katika ngazi zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na miundombinu. Serikali ya Awamu ya Nne, imeendeleza kwa ufanisi mkubwa kazi iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tatu, barabara zinazidi kutengenezwa na kuwa bora zaidi kwa kuwekwa lami na nchi yetu inazidi kuunganika vizuri zaidi kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkoa wa Iringa, Serikali ya Awamu ya Tatu, barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Iringa, ilitengeneza eneo korofi la Kitonga kilomita tisa, sisi wananchi wa Mkoa wa Iringa na Mkoa wa Mbeya, ile sehemu ya barabara hiyo (Kitonga), ni kama lile daraja la Mto Rufiji, bila kutengeneza eneo hilo basi tutakuwa tumetengana kabisa na Makao Makuu ya Nchi ya sasa yaliyopo Dar es Salaam. Lakini Serikali ya Awamu ya Nne, imeendelea kuitengeneza barabara hiyo siyo pale Kitonga tu, mbele kidogo ya Mikumi hadi mbele kidogo ya Mji wa Iringa barabara ile inatengenezwa kwa kutandikwa upya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Iringa, napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kuitengeneza barabara hiyo. Ushauri wangu ni kwamba, barabara hiyo ingeendelezwa kabla huyu Mkandarasi hajamaliza *contract* yake, ingeendelezwa mpaka Mikumi ili iunganike vizuri na ile sehemu ya Mikumi - Morogoro iliyotengenezwa vizuri, kisibaki kile kiraka pale. Lakini pia ninashauri barabara hii badala ya kuishia mbele kidogo ya Mji wa Iringa, Kijiji kinachoitwa Gwachanya, Njiapanda ya kwenda Tosamaganga, ninashauri barabara hii ingeendelezwa kutengenezwa mpaka Mbeya hadi Tunduma, hapo faida za kiuchumi za barabara hii zitakuwa ni kubwa zaidi. Tungeiomba Serikali kwamba Mkandarasi huyu ambaye anaonekana anafanya kazi nzuri basi wangefanya naye mazungumzo ili aweze kuiendeleza barabara hii katika awamu ya kwanza ifike angalau Makambako lakini ifike Mbeya hadi Tunduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya pili ambayo wananchi wa Mkoa wa Iringa tumefurahi sana kuona Serikali imekwishakamilisha upatikanaji wa fedha za barabara hiyo ni barabara inayounganisha Iringa na Dodoma na pia kutoka Dodoma kwenda Babati. Huu ni uamuzi mzuri na naipongeza sana Serikali kwa kufanya jitihada kupata fedha ili barabara hii itengenezwe. Barabara hii ni sehemu ya barabara kuu ya Kaskazini inayojulikana kama '*Great North Road'* inayotoka *Cape Town* mpaka Cairo. Barabara hii, ina umuhimu mkubwa sana kwa nchi yetu, inatuunganisha na masoko makubwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, masoko makubwa ya nchi za *SADC* na pia masoko makubwa unapoelekea kule Cairo ya nchi za *COMESA*. Barabara hii ikiunganishwa vizuri, nchi yetu itaweza kufanya biashara kubwa na masoko hayo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Serikali kwa maandalizi ambayo imekwishayafanya kutengeneza barabara ya kutoka Rujewa, Madibira mpaka Kinyarambo, tumeona harakati nyingi za kukamilisha makisio ingawaje kazi haijaanza. Waziri wa Miundombinu alifika Wilayani kwetu, akatuhakikishia kwamba barabara hii itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami wakati wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa barabara hizi, napenda kuihakikishia Serikali kwamba wananchi wa Mkoa wa Iringa, kwa mara nyingine tena, tutahakikisha ushindi mkubwa kwa CCM kwa asilimia mia moja kama ilivyokuwa katika uchaguzi mkuu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa elimu, napenda kuipongeza sana Serikali kwa kupanua Elimu ya Msingi, Sekondari, Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na kuanzisha Chuo Kikuu cha Dodoma. Huu ni utekelezaji mzuri sana wa Ilani ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ilani ya CCM, imetamkwa wazi kwamba elimu itapanuliwa katika ngazi ya elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya chuo kikuu. Nilimsikia Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Zitto Kabwe akisema *University of Dodoma* ni sera ya CHADEMA, mimi nadhani hapa alijiingiza kufafanua msaafu usio wake, Ilani ya CCM, ni msaafu wa CCM na katika Ilani, imetamkwa wazi kupanua elimu ya Chuo Kikuu na ukisema kupanua elimu ya Chuo Kikuu sasa suala la wapi…

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiangalia saa, naona bado nina *time* kidogo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Endelea.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka ieleweke kwamba katika Ilani hutamki kila *details*, suala la Chuo Kikuu cha Dodoma linaingia kwenye *detail*, napenda kutoa angalizo kwamba tuangalie masuala ya ufanisi katika elimu ya msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo napenda nilichangie kwa kifupi kabisa ni hili suala zima la kukopa mikopo ya ndani ya kibiashara kwa kiwango cha bilioni elfu mbili. Hii inaweza kuleta athari kubwa sana katika uchumi, muda hauniruhusu kuingia katika kuzitamka hizo athari lakini napenda tu nitumie nafasi hii

kuishauri Serikali, iwe kama mtu wa kawaida unapokuwa na mahitaji ya fedha, cha kwanza unachoanza siyo kukimbilia kukopa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ahsante, ni kengele ya pili sasa.

**MHE. JOSEPH J. MUNGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru kwa kunipa nafasi, namalizia kwa kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nami nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwepo mahali hapa wakati huu lakini pia niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Magharibi, walionichagua miaka mitano iliyopita, nikaweza kuwepo mahali hapa, nami naamini nimekuwa nikiwasemea na ninaendelea kuwawakilisha na ninaamini wamekuwa na imani na kazi ambazo tumekuwa tukifanya kwa ushirikiano mkubwa katika Jimbo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu Mawaziri wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu wake na maofisa wote wa Wizara hiyo, ninawapongeza kwa bajeti nzuri ambayo wametuletea hapa, mimi naamini bajeti hii itatuvusha katika mwaka huu wa 2010 mpaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya pamoja na Serikali yake. Nampongeza Mheshimiwa Rais Kikwete, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akifanya na ambayo anaendelea kuifanya na ambayo naamini Watanzania wote watajumuika pamoja kumpa kura nyingi za kumvusha na kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara nyingine tena. Mimi namwomba Mwenyezi Mungu awajalie Wabunge wote walioko hapa, wanapokwenda Majimboni, wote wakabarikiwe na wote warudi salama na Mungu atawajalia mrudi salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme mambo machache. Kuna kitu kimoja nilikiona nikasema lazima nikiseme, nacho ni *balance* kati ya *recurrent expenditure* na *revenue* ya mapato yetu ya nchi hii. Ukiangalia pale *recurrent expenditure* yenyewe iko kwenye shilingi *7.8 million* lakini mapato ni shilingi *6 trillion*. Sasa ukichukua hiyo, ukalinganisha maana yake ni kwamba 1.8 ni misaada itokayo nje. Sasa hiyo mategemeo yake ni kwamba wahisani watatupa fedha hizo kwa wakati lakini kuna tatizo kubwa ambalo wanaliita *"predictability"* kwamba kama hii misaada haikuja kwa wakati, ni dhahiri mipango yote uliyopanga na hata matumizi yote uliyopanga kufanyika kwa kipindi hicho, unaweza usifanikiwe kuyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri hili ni jambo ambalo lazima tuliangalie sana. Hii habari ya misaada, ni jambo kubwa. Sasa hivi ulimwengu mzima wanazungumza habari ya *aid transparency, aid coherence* na mambo mengine, jinsi unavyoweza kulinganisha na kurekebisha utaratibu wa misaada na jinsi tunavyotakiwa kuonyesha

kwamba hii misaada tunaitumia vizuri kwa kazi za maendeleo. Tanzania ni mfano mzuri wa nchi ambayo imekuwa ikipata misaada mingi na sisi kwa kweli tumekuwa tukijitahidi kuitumia vizuri. Nawapongeza sana Wizara ya Fedha, kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini misaada maana yake nini? Misaada maana yake ni hali kubwa ya utegemezi. Utegemezi huu sisi hautusaidii sana kwa maana ya kufika mahali tujitegemee. Kama tunaweza kutumia fedha hizi, zikatuondoa hatua moja, mwaka kesho tukaja tukawaambia Watanzania kwamba sasa tulipofika tumepunguza asilimia 20 ya kujitegemea na mwaka kesho tunaendelea kupunguza, lakini *level* ya utegemezi imeendelea kuwa pale pale, hii ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania tuna rasilimali nyingi, tuna kilimo kizuri, tuna misitu, wanyama wengi, mapato yetu yangeweza kuendelezwa vizuri sana. Nafikiri Watanzania hatuhitaji kuelezwa juu ya rasilimali ambazo tunazo, tunayo madini mengi, misitu mingi, tuna mabonde mengi, kwa mfano mabonde ya Kigoma peke yake tungeweza kuyatumia vizuri, yangelisha nusu ya nchi hii na yangelisha na Burundi yote. Tunachohitaji ni utaratibu mzuri tu ambao utatuwezesha kutumia rasilimali nyingi tulizonazo. Mabonde haya, ni muhimu yakatumika na ni muhimu yakaonekana yana faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini na nakubaliana na wale rafiki zangu ambao wamekuwa wanazungumza kwamba rasilimali zingine nchini ni *sleeping giants*, nilikuwa nafanya kazi na *Canadian International Development Agency* wakati fulani, nikaenda Basuto, kwa kweli nilishangaa sana kwamba *infrastructure* ambayo ingetufanya sisi tujitegemee kwa kulima ngano, leo hii inakufa na katika vitu vilivyokatisha tamaa Ubalozi wa Canada ni *infrastructure* ile kuachwa hivi hivi. Lakini taratibu na misaada ambayo tumepata iko mingi ambapo tungeiendeleza ingeweza kutusaidia sana. Hivi kwa nini hatutaki kujitegemea katika kilimo cha ngano wakati tuna *import* ngano nyingi sana na tungeachana na ngano ya kutoka nje.  Maana ngano ingeweza kutusaidia sana. Yako mambo mengine hatuhitaji mtu kutoka nje aje kutufundisha, ni mambo ambayo sisi wenyewe tunayafanya na tumeyafanya toka utoto wetu wengine tunayaona tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo chetu si kilimo kikubwa kinahitaji *transformation*. Sasa tunazungumza habari ya *power tillers.* Kwa mfano, Kigoma tuliambiwa *power tillers* itauzwa kwa shilingi milioni nne mpaka sita lakini inafikia shilingi milioni tisa mpaka 10, hizi gharama zimetoka wapi? Naomba Waziri atakapokuwa ana-*wind up* pengine nielezwe tu hizi gharama nyingine kama ni gharama za Halmashauri kushughulikia maana zimekuwa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitoe tu tafadhali kwamba katika utaratibu wa bajeti yetu hii, kuna mambo nayaona ni makubwa sana, moja ni hilo la uchaguzi ambao *obviously* litachukua gharama kubwa lakini la pili, ni hilo la Vitambulisho vya Watanzania ambavyo tunavihitaji sana lakini la tatu ni mishahara kupanda. Katika uchumi wa kawaida, ukifanya yote haya kwa pamoja lazima utapata tatizo. Kwa hiyo, hii

ni *caution* tu natoa haya mambo matatu yana *pressure* au *very high demand on public expenditure*, yote haya yanafanywa katika bajeti ya mwaka mmoja. Kwa hiyo, lazima tukubali kwamba baadhi ya matumizi mengine itabidi *at some point* yaweze kusitishwa, haitakwenda kama ambavyo inafikiriwa. *Of course*, jinsi inavyo-*feed back* kwenye *economy*, matatizo yapo, hatutayakwepa, tuwe tayari kwenda kuhakikisha kwamba *as much as borrowing from the banking system* inakuwepo liko tatizo ambalo litajitokeza na hilo tatizo mimi naamini Wizara ya Fedha ina watalaam wazuri na sasa Wizara ya Mipango, wataalam hawa watasaidiana kuangalia na kuhakikisha kwamba *process* nzima hii haiwi *inflationary*. Nalisema hili kwa kuelewa kwamba hayo yote lazima yatakuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali yetu na hasa tunapofikiria bajeti nzima kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni hili ambalo linawahusu wananchi wetu kule vijijini. Sehemu nyingi kuna migogoro ya mipaka na hiyo ninaomba Wizara inayohusika iliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, ninaunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM MUHAMMAD SANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mola, kwa kunifikisha salama na kupata nafasi hii ya kuchangia siku hii ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, niwashukuru wapiga kura wangu wote wa Mji Mkongwe, kwa kuonesha imani kubwa sana juu yangu kwamba nilifanya na naendelea kufanya kazi zao katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na Jimboni kwangu na kwa kuridhia tena niwe mgombea na kilichobakia sasa hivi, kama itawezekana hata niapishwe kabisa kabla ya huo uchaguzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka nizungumzie kidogo kuhusu namna gani tunaweza tukawasaidia wavuvi. Sikatai bajeti kuelekezwa kwenye kilimo, ndiyo uti wa mgongo. Asilimia kubwa ya wananchi wetu wanazalisha chakula kwa ajili yao na kwa ajili ya ziada ya kusafirisha nchi za nje lakini mvuvi kapewa nafasi gani? *Initial capital* ya mkulima inaweza ikaanzia hata shilingi 100,000 na kuendelea, inategemea na kilimo chake lakini mvuvi anahitaji si chini ya shilingi milioni 10 kuanzisha mradi wa uvuvi wa chini kabisa yaani kununua boti, kununua mashine kama Yamaha ambayo takribani inafika shilingi milioni 3.5, hizo ndizo fedha anazozihitaji. Hakuna *incentive* zozote zilizoonyeshwa na Serikali kwamba walau tupunguze viwango vya ushuru au kuondoa kabisa katika suala hili la uvuvi. Kutoka kijiji cha Moa mpaka Msimbati yaani kutoka Tanga ukanda wa mpaka Msimbati, Mkoa wa Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara karibu Wilaya tisa zina vijana wanaohitaji uvuvi wa kisasa ambao utawapa ajira wao na kuongeza mapato Serikalini. Sasa basi uvuvi haukwenda hapo tu hata kwenye maziwa yetu Mwanza, Rukwa, Mara, Kigoma, Bukoba, Mbeya mpaka Ruvuma ukiangalia Wilaya zote hizi si zaidi ya Wilaya 22 hivi, Serikali inashindwa nini hadi leo hii kutenga walau dola milioni 22 kwa mwaka mmoja tu kwa kila Wilaya wakapata dola milioni moja ili kuendeleza uvuvi huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yamezungumzwa sana na Mheshimiwa Mudhihir, yamezungumzwa sana na Mheshimiwa Mongella, yamezunguzwa na Mheshimiwa Shah, yamezungumzwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, yamezungumzwa na Mheshimiwa Manju Msambya, kwa sababu uvuvi hauko kwenye maziwa tu. Leo tunasafarisha tani ngapi kutoka *Lake Victoria* kupeleka Ulaya? Hatuwezi kuingia bahari kuu kwa sababu gharama zake ni kubwa, vifaa vyake ni ghali, lakini hebu tuwawezeshe hawa wavuvi wadogo wadogo kuwapatia misaada hii ya fedha wakaweza kujiendeleza, wakavua kwa faida yao wenyewe, wakaingiza mapato katika Serikali na ikawa ni sehemu ya kupata chakula kilichokuwa na *protein* katika ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema Serikali hii inakusanya zaidi ya shilingi bilioni 350 kwa mwezi, hivi kutenga dola milioni 20 mpaka 22 kuwapatia vijana hawa, tunashindwa? Hizo ndizo ajira, hawa wakishajiajiri wenyewe, kikapatikana hicho kipato wataji-*engage* katika mambo mengine, watakuwa na vikundi vyao vya uvuvi. Tukiwaacha na kuwanyang’anya nyavu zao ndogo ili wasivue, wataanza kuingia kwenye mashamba ya watu waibe mahindi maana hawana la kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Tanzania tuna tabia ya kutaka makubwa, tuanze na mambo madogo. Hivi tunazalisha pamba nyingi sana lakini hatutengenezi vitambaa. Hadi leo hii miaka 40 ya uhuru nguo za Wanajeshi wetu, Polisi, Magereza zinaagizwa kutoka nchi za nje. Twende Syria tukaone wanafanya nini na pamba yao. Twende nchi ya *Egypt* tukaone wanafanya nini na pamba yao, tuwachukue wataalam kutoka India, Thailand, tunao vijana wa JKT washone nguo za Jeshi la Polisi ili tuhifadhi fedha za kigeni badala ya kuagiza nguo za Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi Tanzania kutoka nchi za nje. Afrika Kusini wanajitegemea na nguo za vikosi vyao. *Egypt* na *Syria* wanajitegemea, kwa nini sisi tusijitegemee? Tubakie kuuza korosho ambazo hazijabanguliwa, tuuze pamba tusitengeneza viwanda vidogo, kwa nini? Tutapata ajira kwa ndugu zetu, ambao watatoa hizo nguo kwa ajili ya sare za Majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, angalieni bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani, chekecheni muoni kiasi gani cha fedha za kigeni tunazoagiza nguo za Polisi, nguo za Wanajeshi, nguo za Magereza ili tutengeneze wenyewe. Pamba ipo Mwanza ya kutosha lakini tuna zile ndoto za nadharia, tuna *Uranium*, watu walishaanza ku-*predict* mambo ya ajabu ajabu, sijui umeme tutapata rahisi, *Uranium* ina matatizo, ina Sheria zake za Kimataifa, tunao watalaam wa *Uranium*, si zaidi ya wataalam 10, kiwanda kidogo tu cha kufua umeme wa *Uranium* kinahitaji wataalam 100 mpaka 150 waliobobea, leo utakwenda kuwachukua watu wa nchi za nje waje wasimamie kiwanda ambacho kinazalisha umeme kutokana na *Uranium*, hatuwezi, tuwaelimishe watu wetu kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalizungumzwa na Profesa Mkilaha mtaalam wa mambo ya Uranium, alizungumza hili kwamba hatuna watalaam wa kutosha, tuwaelimishe watu wetu kwanza, tuache *Uranium* na hayo mambo mengi tumeyavamia ndio tukafika hapa tulipo. Ilikuwa sisi hatuna haja ya dhahabu, hatuna haja ya *Uranium*, kilimo, ufugaji, utalii na bahari kuu, haki ya Mungu ingeendesha bajeti ya Tanzania na tukawa na fedha za ziada, lakini wapi tunabuni tu mambo. Watu wa kutaka ushauri wapo,

hebu nendeni kwa Profesa Lipumba mkachukue ushauri, ni Mchumi mzuri tu anaweza akasaidia nchi yake hii. Kwa nini anachukuliwa na nchi za nje tusimtumie sisi? Muwahini Profesa Lipumba kabla hajafanya vitu vyake mwezi Oktoba *otherwise* tutakuja kuathirika hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania lazima ijikite katika masuala madogo madogo, makubwa tuyaweke kando kwanza. Tusafirishe bidhaa ambazo zimetengenezwa, tuchukue matunda ambayo tunaweza tukasafirisha *juice*, korosho tupeleke ambazo zimebanguliwa, pamba tutengeneze nguo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Uandike kwa maandishi.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba anaendelea kuniimarisha na naamini nitaendelea kuimarika baada ya tukio langu gumu na ninaamini ni hali ya kidunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, napenda nichukue nafasi hii, kwanza kabisa na mimi kuwashukuru Wanawake wa Mkoa wa Mwanza. Wanawake wa Mkoa wa Mwanza walinipenda, wakaniwezesha kuingia katika Bunge hili kwa muda wa miaka mitano na mimi ninawapenda hadi sasa na ninaamini wataendelea kunipenda ili niweze kuendelea kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuipongeza Halmashauri ya Jiji la Mwanza, kwa usafi wa Jiji hilo hadi leo tunaendelea kuongoza, kwa awamu tano mpaka sasa. Kwa kweli nasema hongereni sana Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango mzima wa bajeti, mara nyingi maeneo ya wafugaji huwa wala hayatajwi kabisa. Hata hivi sasa vipaumbele ni vizuri tu elimu, miundombinu, afya na vinginevyo lakini tusipozungumzia Wizara zingine hizi zinazobaki, inaonekana kama vile basi zinatupwa kapuni kabisa. Ukiona mwendelezo mzima katika matukio kwa mfano wenzetu wavuvi wanatetewa sana, wengine ambao wanaweza kutetewa ni wananchi ambao wanapata matukio kwa mfano ya mafuriko, wanabebwa haraka sana, lakini wafugaji jamani, ng'ombe wake wote wanakufa, anabaki mtupu lakini mbona Serikali huwa haishtuki haraka? Mimi sijaona Serikali inakwenda rasmi kwamba hawa ng'ombe wao wamekufa hawana hata mmoja, kwa mfano, Wamasai wanakosa maziwa, wanakosa nyama na ndio chakula chao. Sasa niwaombe wafugaji hebu mjikite kikwelikweli mtakapopata nafasi ya kuongelea ndani ya Wizara muone bajeti inazungumzia nini kuhusu wafugaji ambao hawana msaada kabisa na wengine wanafikia hata kupoteza maisha kwa sababu hajui tena ashike wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Zaidi sana naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunijalia afya ya kuweza kusimama hapa tukiwa tunaelekea kukamilisha miaka mitano hii ya uhai wa Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze wanawake wote nchini na hasa wa Mkoa wa Kagera kwa namna walivyochangia maendeleo kwa kumudu kuweza kulea jamii ya Watanzania, lakini pia wakiwa wahimili wakubwa wa uchumi kupitia kilimo. Kwa asilimia kubwa huko vijijini wanawake ndio wakulima na kwa kweli inatia moyo sana na wanastahili pongezi kwa kuwa mazao wanayolima yanavuka hata mipaka ya mkoa wa Kagera; ndizi, maharage, udaga, mchele na mazao mengine yanauzwa hata nchi za nje. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi napenda niwapongeze lakini niiombe Serikali kwamba wanawake hawahitaji kitu kingine zaidi kuliko kupewa mazingira mazuri ya kufanya kazi pamoja na kutatua matatizo yao ya kawaida, wakienda hospitali wakute dawa, watoto wakienda shule wakute vifaa vya kutosha na mazingira mazuri ya kusoma na mambo mengine kama usafiri ili kuweza kusafirisha mazao yao na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru sana wanawake hasa wanachama wa UWT, kupitia Chama cha Mapinduzi ambao waliniwezesha kuwawakilisha katika Bunge hili na sasa tunapoelekea nina hakika kabisa wapo tayari kuniunga tena mkono. Kwa hiyo, ninazidi kuwashukuru sana nikiwaombea amani ya bwana iendelee kuwa pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri sana ya kujenga uwanja wa ndege wa Bukoba. Kazi inayofanyika ni kubwa na ni nzuri sana na nimefarijika sana na kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Kagera, mimi ninaomba nishukuru kwa maana hata katika Bajeti hii, tumetengewa shilingi bilioni 11.769 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo. Nina imani huu uwanja utaendelea kujengwa hadi kufikia kiwango cha lami, kwa sababu bila hivyo kwa kweli itakuwa ni ngumu kwa sababu sehemu ile ina mvua nyingi kwa hiyo, ikiishia tu kwa kiwango cha changarawe haitatusaidia sana. Lakini pamoja na hayo kwa hatua tunayoendelea nayo, mimi naipongeza sana Serikali, kwa kweli wananchi wa mkoa wa Kagera, tumefarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi hii nzuri ya kujenga uwanja wa ndege wa Bukoba, kumejitokeza tatizo kubwa na athari kubwa baada ya barabara iliyokuwa inakwenda maeneo ya Kashai, Nyamukazi na Kahororo, kufungwa ili kupisha ujenzi wa uwanja huo. Maeneo haya niliyoyataja yanafikika kwa shida; barabara inayokwenda kule inazunguka sana, lakini pia ni nyembamba. Sasa kama kweli ni barabara ambayo inaweza hata ikapitisha magari makubwa kwenda katika maeneo hayo, nadhani itabidi barabara hiyo ipanuliwe, lakini ili kupanuliwa itabidi baadhi ya nyumba za watu kuvunjwa. Sasa mimi ninapoingalia Manispaa ya Bukoba naona kwa kweli kazi hiyo itakuwa nzito na itakuwa nje ya uwezo wao. Kwa hiyo, mimi naomba Wizara ya Miundombinu iangalie namna ya kushirikiana na Manispaa ya Bukoba ili barabara hii iweze kutengenezwa

vizuri na wananchi waweze kupita vizuri bila matatizo yoyote, kwa sababu tayari ajali mbalimbali zimeanza kujitokeza kwa sababu ya kupishana katika hii barabara ambayo ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie jambo la mwisho kuhusu barabara ya Katoma kwenda Kanyigo, eneo la Akaja. Eneo hili limekuwa ni kero, mvua nyingi zinaponyesha basi barabara hiyo inafungwa na kwa hiyo, watu wanaokwenda Kanyigo hawawezi kupita mpaka wazunguke maeneo ya Bugandika mpaka Bwanja ndipo waende na barabara inakuwa ni ndefu sana. Hii imekuwa ni kero ya muda mrefu, tumeizungumza katika bodi ya barabara ya mkoa lakini hatupati ufumbuzi kwa vile inaelekea fedha inayotengwa kwa ajili ya barabara hii inakuwa ni kidogo sana.

Kwa hiyo, mimi naomba suala hili liangaliwe, barabara hii imekuwa ni kero sana na hata wakati mwingine watu wanakwazika kwa sababu inawabidi wazunguke mwendo mrefu sana kwenda katika maeneo wanayotaka kwenda pindi barabara hii inapofungwa mvua nyingi zikinyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa niliandaa kuzungumza mambo machache na nina nidhamu, ninaomba nikushukuru tena na niseme kwamba ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala,* kwa kutuwezesha sisi sote kuwa salama na wazina na kushirikiana katika mjadala wa leo katika Bunge hili. Vilevile niwashukuru wanawake wa mkoa wa Dodoma, kwa kuniwezesha kupata nafasi hii ya kuwawakilisha Bungeni na ninaamini mimi ni mama yao wananifahamu na wataendelea kuniamini hata kwa kipindi kinachokuja. *(Makofi).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayoifanya katika Mkoa wa Dodoma. Moja ni kuhusu barabara hii ya kutoka Dodoma – Babati na Dodoma – Iringa; tunaishukuru Serikali imekuwa inatueleza maelezo mazuri na tunayaamini na ninaamini kwamba mpaka sasa kama walivyosema kazi ya kuanza ujenzi wa barabara hizi haitachukua muda mrefu ila tu wananchi wa Mkoa wa Dodoma wananchoomba ni kauli za kwamba zina makandarasi, wataanza wakati wowote, zimechukua muda mrefu. Tunachoomba sasa ni basi makandarasi hawa kama wameshawekeana mkataba na Serikali basi kazi ianze ili wananchi wa Mkoa wa Dodoma wawe na imani na Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nililoliona kwenye Bajeti hii ni kwamba barabara ya kutoka Dodoma – Babati, tunaamini Serikali imetenga hela za kujenga barabara hiyo, lakini kwa kipindi hiki cha mwaka 2010/2011, naona kwamba imetengewa shilingi bilioni tisa. Sasa pengine ni vizuri tukapata maelezo ya kuhusu suala la makandarasi ni kwa nini wanachelewa na vilevile hizi shilingi bilioni tisa, zimetengwa kwa ajili hasa, ya kufanyia nini? Kwa sababu tunaamini barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami na kwamba kiwango hicho kilichotengwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ningeomba nizungumzie suala la kilimo. Sisi wa mkoa wa Dodoma, tuna mazao ya chakula na ya bisahara, sasa tungeiomba Serikali iweke mkazo na hasa kuhusu suala la kilimo cha zabibu, mazao ya biashara ambayo ni zabibu, karanga na ufuta. Serikali ijitahidi angalau kuwashawishi wale ambao wanaweza kuwa wawekezaji kwa ajili ya kutuanzishia viwanda vidogo vidogo vitusaidie kusindika mazao haya na hata ikiwezekana basi hizo mashine ambazo ni za kusindika mazao haya, ikiwezekana basi wanaweza wakashawishiwa wakazileta Dodoma na wananchi walio na uwezo wakazinunua ili kuanzisha viwanda hivyo vidofo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu, hakuna anayebisha kwamba Serikali imejitahidi kusimamia Ilani ya Uchaguzi na kwamba shule za sekondari zimejengwa, za msingi zimeboreshwa na sasa kilichobaki kwa Serikali kwa kushirikiana na wananchi ni suala zima la kujenga nyumba za walimu na ambacho kwa kweli ndicho kinachozuia hata walimu wakipangiwa baadhi ya shule wanaweza wakaondoka wakaenda katika maeneo ambayo wanaweza wakapata nyumba za kuishi na wakafanya kazi vizuri.

Vilevile suala la maabara ili tuweze kupata wanasayansi na pia kujenga hosteli kwa ajili ya wasichana wetu. Ni sawa vijana wa kiume na wa kike lakini hasa wasichana kwa sababu tunaamini kwamba tatizo kubwa walilonalo wasichana ni lile la kupata mimba. Kwa hiyo, wakiwa na hosteli angalau idadi hiyo ya wasichana kupata mimba inaweza ikapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala ambalo kwa sasa hivi ni mpango wa Serikali wa kujenga barabara ya kutoka *keep left* ya Shabiby kwenda kuunganisha na barabara inayotoka Arusha, na kwamba barabara hii imepita katika nyumba za watu na kuna nyumba zimewekewa alama *X*, tayari kwa kuvunjwa. Lakini yapo maneno ambayo sijui kama ni sahihi yanayosema kwamba nyumba hizo zitakazovunjwa hazitalipwa fidia; basi tunaiomba Serikali itusaidie kutupa maelezo, kwa sababu hatuna uhakika kama maneno haya ni ya kweli ama si ya kweli. Tunaiomba Serikali itueleze na wananchi waweze kusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa muda ni mfupi, nimeona niguse mambo ambayo kwa kweli nimeona yana umuhimu katika mkoa wa Dodoma. Lingine ni kuhusu ujenzi wa kiwanja cha ndege, nimeona umetengewa hela kidogo; sasa sijui hizi hela ni za kufanya nini? Mkoa wa Dodoma kama mnavyouona na hasa mji wa Dodoma, unakuwa na unahitaji mambo mengi yawe yamekamilishwa. Tusipofanya hivyo sasa hivi nadhani baadaye tunaweza tukaendelea kupata shida na pengine hata ujenzi wake unaweza ukawa ni mgumu. Niiombe sana Serikali iweze kutenga fedha za kutosha miaka inayofuata na kuanza ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Dodoma ambacho ni kiwanja kikubwa na ninaamini Serikali inalijua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wa Dodoma una kituo cha mabasi ambacho wote nadhani mnakifahamu na pia tuna kituo cha daladala; vyote hivi sasa hivi vimekuwa ni vidogo, daladala zimejaa na zinashindwa hata kusimama kwa muda mrefu. Vilevile

mabasi yamejaa na vyote hivi vimejaa; tunaomba uwanja upo lakini hatuelewi ni kitu gani kinachozuia ujenzi wa uwanja huu wa kituo cha mabasi makubwa na vilevile kuandaa kituo cha mabasi madogo ya daladala.

Sasa pengine hili nalo ningeomba nipate maelezo ya kwamba Serikali inalionaje? Imelisahau au ni vipi? Lakini ninaamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu na inajitahidi kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Ninaamini pengine mpango upo, tunaomba tu tupate maelezo ili tuweze kufarijika ni vipi Serikali inayashughulikia matatizo yanayowahusu wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja. Ya pili, nitoe shukrani kwa Serikali na hasa Wizara zinazoshughulikia barabara, njaa, kilimo na maji, kwa kazi kubwa ambayo zimekuwa zikifanya katika wilaya ya Jimbo langu la Rombo, hii miaka ya karibuni na hasa mwaka uliopita na hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia mambo mawili. La kwanza ni maswali *(a), (b), (c).* La pili ni suala la *MKUKUTA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maswali, nataka kumuuliza Waziri wa Fedha labda atusaidie, ni kwa nini katika taarifa hii hatujapata maelezo ya mafanikio tuliyoyapata baada ya kuteremsha kiwango cha kodi ya *VAT* kutoka 20 hadi 18, tumefanikiwa kiasi gani? Kwa sababu labda swali hili litatoa mwanya kwa *Finance Bill* ambayo tutaijadili baadaye, suala la *VAT* nalo liko pale. Sasa kwanza mwaka jana baada ya kuteremsha, tumefanikiwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwa nini, kitabu cha mipango na cha fedha; hotuba mbili hizo hazitaji hata mahali pamoja uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo, hata mahali pamoja? Ukichukua Bajeti ya sasa, ukiondoa tu kwamba kuna *SIDO* imepewa fedha pale kupitia Wizara yake ya Viwanda na Biashara, ukichukua mpango wa muda wa kati *(medium term),* mpaka mwaka 2013/2015 viwanda vidogo havitajwi kabisa. Je, Sera na Ilani ya Uchaguzi ya Chama juu ya viwanda vidogo ndio basi tumefika mwisho? Kama ndivyo, hili jambo linasikitisha na siwezi kuliunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu; hivi Waziri na wenzake wanafahamu kwamba nchi nzima haina vipimo, inafanya biashara bila vipimo? *Weight and measures,* nchi nzima! Ndio maana watu wanaingia vijijini, wakulima wanauza mazao kwa lumbesa, kwa sadolini na maneno mengine ya aina nyingi; nenda kwenye duka lolote leo ile mizani wanayotumia kwanza ni ya zamani mno, haina vipimo sahihi na mambo kama hayo. Tatizo hili linaeleweka Serikalini, lakini halijaamuliwa sawa sawa. Mimi nauliza tu, ni nchi gani duniani inafanya biashara bila vipimoTanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye mada yangu kubwa, *MKUKUTA.* Mimi ni kati ya watu wenye wasiwasi mkubwa kabisa kwamba hata huu *MKUKUTA* wa

pili hautafanikiwa; ni kweli na wala tusizungumze kidiplomasia hapa, *MKUKUTA* wa kwanza haukufanikiwa, *MKUKUTA* wa pili nahisi hautafanikiwa. Hautafanikiwa kama utaendeleza mambo yale yale tuliyoanza nayo *MKUKUTA* wa pili; yaani Waingereza wanasema *old wine in new bottles,* kama tukiendeleza *old wine in new bottles,* hatutafanikiwa. *(Makofi)*

Mimi nafikiri sababu yake kubwa ni kuwa tumejishughulisha mno na *stuctures*, hela nyingi mno ziko kwenye mifumo na utawala na *D by D* na vitu vingi vya namna hiyo ambavyo havimlengi mlengwa wa *MKUKUTA* ambaye ni kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulenge tu pale kwenye kaya tukajiuliza maswali, huyu mtu wa kaya, anahitaji nini? Kwanza anahitaji aongeze uchumi wake, huko kwenye kilimo na mifugo na uzalishaji wa viwanda vidogo na biashara, ndio uchumi wa mwanakaya uko pale, kila mtu na wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tungetumia fedha za moja kwa moja *(direct financing)* ya maeneo yale ya kuongeza uchumi wa mwanakaya na tukafanya kwa miaka hii mitano ya *MKUKUTA* tunayozungumza nina hakika nchi hii itabadilika lakini sivyo ilivyo sasa hivi na ndiyo maana nina wasiwasi kwamba kama hatuwezi kuongeza uchumi wa kaya moja kwa moja hakuna namna maana yake ni kilimo kwanza lakini lazima kiwe ni kilimo cha namna gani, ruzuku kwa mbolea, kwa miche, kwa mbegu, dawa na zana nyingine nyingi zinazotumika kwenye kilimo na ufugaji na uvuvi. Bila hivyo mimi kabisa naweza nikawahakikishia kwamba tutakapofika hapa hatutaonyesha maendeleo makubwa ya kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye kaya la kufanya somesha mwanakaya, msomeshe afanye vizuri zaidi vitu anavyofanya sasa hivi kama ni mifugo afuge kwa njia bora zaidi kama ni kilimo alime kwa njia bora zaidi maana yake hii ni *extension.* Lakini somesha na watoto wa mwanakaya huyu maskini tunayemzunguzia ndiyo lengo la *MKUKUTA* tusomeshe watoto wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi watoto wengi pamoja na kwamba tumeteremsha sana ada kwenye shule za sekondari, watoto wengi bado wanashindwa kulipiwa ada na wazazi wao. Hivi ni kitu gani tunashindwa kabisa kuhesabu watoto hawa na kuwasomesha bure hata mpaka Chuo Kikuu, wale maskini sana *(the poorest of the poorer)* ndani za jamii zetu watoto wao wasomeshwe bure mpaka Chuo Kikuu na hasa tungekuwa tunajitutumua sawa sawa tungesema elimu ya bure kwa sekondari. Lakini najua Waziri wa Fedha nasema kama huwezi elimu bure katika sekondari tuchukue wale watoto wa watu maskini sana tuwasomeshe bure mpaka Chuo Kikuu wala sio sekondari tu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, jambo la pili, kwanza inua uchumi, somesha mtoto wa maskini na yeye maskini mwenyewe mpe elimu ya watu wazima ili aweze kufanya kwa ubora zaidi yale mambo ambayo anafanya sasa hivi. *(Makofi)*

La tatu mpe maji, mtafutie maji karibu kabisa huyu maskini muda mrefu mno akina mama wanatumika kufuata maji, watoto wanafuata maji, na maji yako mbali na yakiwa mbali ni machafu. Tufanye kila namna njia mojawapo ni kuvuna maji ya mvua, kila maji ya mvua kuna baadhi ya miji duniani humu hupewi *building permit* kama huvuni maji ya mvua ndani ya miji. Mji mmoja ni madrasa siku hizi unaitwa Shelai, pale huwezi ukapata kiwanja na ukajenga kama huvuni maji ya mvua kwenye nyumba yako. Lakini leo uvunaji wa maji ya mvua kwenye mapaa yetu maji ya mvua yanatiririka hakuna mtu anayeyashughulikia kikamilifu, mpe maji mtu maskini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya ahsante, tunashukuru.

**MHE. BASIL P. MRAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naiunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza na mimi nianze kwa kushukuru kwa Bajeti hii tuliyoletewa ambayo kwa kiwango kikubwa nikiangalia nadhani haitofautiani sana na Bajeti ya mwaka jana. Kwanza nasema hivi ukiangalia hili ongezeko la Bajeti kwa ujumla za matumizi ya kawaida na ya maendeleo. Bajeti ya maendeleo mwaka jana ilikuwa asilimia 30, mwaka huu ni asilimia 34 lakini hili ongezeko *in real terms* sio ongezeko kwa sababu ukichukulia *element* ya *inflation* hata na mambo mengi ya thamani ya pesa inakuwa *negative*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ukiangalia sana lile ongezeko la kutoka trilion tisa kwenda trilion 11 nikiweka maanani vigezo vya mfumko wa bei unakuta pia inanipa ongezeko lililo chanya yaani *negative*. Kwa hiyo, kwa ukweli ni kwamba ni Bajeti ambayo ni sawa tu naweza kusema kwa kiwango kidogo inataka kufanana na mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo moja limeanza kutuondoa kwenye msingi wa utawala bora. Mfumo wetu wa demokrasia unazingatia uwakilishi na uwakilishi huu unatakiwa uende kwenye ngazi zote kuanzia kwenye ngazi za kijiji ambako wana utawala wa moja kwa moja ambako wanatakiwa wanakijiji wote hao wananchi kwenye mkutano mkuu wafanye maamuzi yao ya msingi hadi Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye utaratibu wetu Serikali yetu ina uwakilishi wa wanasiasa, watu ambao wanawakilisha wananchi. Sasa huu mtindo ulianzishwa ambapo Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ameizungumzia sana wa kuanzisha *executive agencies*, kuanzisha *authorities*, kuanzisha *commissions* tunahama kwenye *representative democracy* tunaenda kwenye *technoclass* yaani utawala unaotumia wataalam kuiendesha nchi. Sasa hili ndiyo hilo linatuletea matatizo ya kawaida tunayoyaona ya kwamba wataalam usitegemee watasikiliza sana maombi au maoni ya *organization* kama *CTI* au *TCIA*. Kwa sababu ukiangalia sana jambo moja ambalo litaweza kutumiwa na wataalam, ni kengele ya mwisho au?

**NAIBU SPIKA:** Bado moja.

**MHE. DR. ANTHONY M. DIALLO:** Samahani, kwa hiyo, wataalam watakachoangalia mfano kwenye kutafuta kodi, ni kila mwaka wataangalia bei ya sigara, bei ya vinywaji na mambo mengine na sasa hivi wanaangalia na magari. Kwa sababu ndiyo vitu ambavyo wanaweza kuvipata kirahisi, wanaacha kuangalia mambo mengine ambayo kwa kuzingatia utaratibu ule wa *representative democracy* tulikuwa nao. Mfano mmoja ni tunapoanzisha haya ma-*organization* ma-*executive agency* kinachotokea ni kwamba wanamnyang'anya Waziri wa Fedha zile pesa tunazi-*intrust* kwenye bodi, bodi ambayo kwa sasa hivi kwa bahati mbaya tena tumetunga sheria wanasiasa hawaruhusiwi kuingia, hata kwenye ngazi ya Halmashauri wanasiasa walikuwa zamani wana maamuzi kwa mfano kwenye mfumo wa manunuzi sasa hivi madiwani hawaruhusiwi. Kwa hiyo, kinachotokea ni huu mfumo wa *technoclass* ambao wataalam ndiyo wanaiendesha nchi. Sasa tutafika wapi, nadhani hilo tunatakiwa tuliwaze mara mbili. *(Makofi)*

Sasa mimi nina hakika *executive agencies* au haya mashirika mengine yangekuwa na kodi, kwa sababu kwa sasa kwa bahati mbaya sana Waziri wa Fedha hapati hata *dividend* kutoka kwenye haya ma-*executive agency*, wakati wanatengeneza faida. Zile faida wanazitumia kwenye kutembea wanakwenda semina, hata kama ni ya saa moja watakwenda.

Sasa utaratibu unaotumika ukiziangalia *executive agencies* zote hizi na mashirika haya tuliyoyaanzisha *they so called authorities* wana mabilioni ambayo sikuona umuhimu wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kupandisha hata bei ya sigara au kupandisha bei ya bia au nini, ungewaambia tu wakakupa hata *five percent* ule *short fall* au ule upungufu ambao ungeipata kwenye Bajeti ungeipata kutoka kwao. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali tuangalie upya utaratibu wetu huu kwa sababu fedha ambazo zilitakiwa ziwe masurufu kwako sasa hivi zinatumiwa na bodi kwa maamuzi ambayo hayahusishi wanasiasa. *(Makofi)*

Sasa tutakwenda vipi, tutafika mahala hata hili Bunge tutakuwa tunafanya maamuzi kwa sababu tunaoi-*run* nchi sio, sisi tutafika mahali tutakwama. Kwa hiyo, naomba sana Serikali mliangalie hilo, utaratibu huu hata kwa nchi ambayo walioanzisha Marekani wa *regulation* siku hizi wanaimba *de-regulation* na wao wanaufumua wamebaki kwenye maeneo machache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuzungumzia kuhusu suala la ruzuku, ruzuku naomba kwa kifupi sana tuhusishe mazao yote ndiyo tutapata *agregated value added* la sivyo tuta-*concetrate* tunahangaikia na zao moja tunaacha mazao mengine ambayo huenda pengine faida kwa nchi ni kubwa zaidi kuliko tunayohangaikia. Kwa hiyo, ruzuku ihusishe pamba, karanga, alizeti na kadhalika pale ndiyo tutapata faida ambayo tunaitarajia. *(Makofi)*

Mwisho nirudie Mwanza tunahitaji *Internationa Airport* la sivyo kuwa na *airport* moja siku tutakapopata tatizo kama juzi juzi hapa tulipata matatizo ya barabara kidogo tu watu ikabidi wahangaike tena kurudia kupitia Nairobi kupitia Moshi na kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo, *International Airport* sio kwa suala la kibiashara tu lakini itasaidia

sana kuwa inatumika kwa muda wote wa saa 24 ndege zinaweza kuruka na kutua na itakuwa na manufaa makubwa kwa kuleta bidhaa ukiacha suala la abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nizingatie muda mfupi tuliopewa naunga mkono hoja kama marekebisho haya mliyoyasema na mapendekezo yatachukuliwa kama nivyoomba. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwanza kabisa naomba niwashukuru wote waliopewa nafasi ya kuchangia kwa siku hizi mbili na tunategemea siku ya Jumatatu Mawaziri waliguswa na michango ya Waheshimiwa Wabunge katika hotuba hii ya Waziri wa Fedha wajiandae ili waweze kuanza kutoa majibu kwa dakika zao kumi na tano zile. Kusudi Waziri mwenyewe ajibu yale mambo yake ya kisera.

Kwa hiyo, tuna wachache tu watakaoingia siku ya Jumatatu asubuhi kama watakuwepo, halafu Waziri, Naibu Waziri, halafu Waziri mwenyewe. Kipindi cha jioni ya siku ya Jumatatu tunapenda Wabunge wote wawepo hapa kwa sababu tutapiga kura ya mtu mmoja kukubali au kuikataa Bajeti hii. Kwa hiyo, popote waliko Wabunge lazima wawe wamerudi siku ya Jumatatu kipindi cha jioni kwa sababu hicho ndiyo tutapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matangazo machache, bahati mbaya utaratibu wa Jumamosi hata kutambulisha wageni haujui unaingilia wapi lakini nadhani wageni waliokuwepo wengine wameshaondoka. Ila naamini Katibu Mkuu wa KKKT bila shaka yupo ndugu Madi, nadhani, kwa nini huyu nimemtaja huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Kepteni John Chilligati lakini na Wabunge wote wa mkoa wa Singida kwa sababu leo jioni saa moja na nusu kuna chakula cha hisani kilichoandaliwa na kanisa la KKKT Dayosisi ya Kati kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Singida. Kwa hiyo, naamini Wabunge wengi wamekaribishwa na mnakaribishwa tena. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hivyo pia kwa sababu asubuhi tumeanza na kuwasilisha Muswada wa Fedha kwa kusomwa mara ya kwanza. Kwa hiyo, Kamati inayohusika inabidi ikae kuweza kupitia Muswada ule, kwa hiyo Mwenyekiti wa Kamati hii Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake hiyo ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwamba kesho tarehe 13 kutakuwa na kikao cha Kamati kuanzia saa tano asubuhi katika ukumbi namba 231 hii ni ghorofa ya pili. Kwa hiyo wajumbe wa Kamati hii na wengine wanaopenda si lazima lakini wao ndiyo wenye maamuzi lakini na Wabunge wengine pia wanaweza kushiriki kwenye Kamati hiyo saa tano kesho ukumbi namba 231 ni vizuri kushiriki kwa sababu katika Kamati mnaweza kufanya mabadiliko makubwa haya yaweze kufanyiwa katika ngazi. Kwa hiyo, hata Wabunge wengine wanakaribishwa lakini rasmi wajumbe wa Kamati hiyo kesho saa tano asubuhi kwenye chumba namba 231. *(Makofi)*

Baada ya matangazo haya Waheshimiwa Wabunge naomba niwashukuru kwa wikiendi hii, nadhani leo mtaweza kuangalia mipira hiyo bila matatizo makubwa, jana tulipata matatizo kidogo lakini niwatakie wikiendi njema na mpumzike kwa salama. Basi naahirisha kikao cha Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 6.25 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu, Tarehe 14 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)*